Haliuzwi
MACHI 30, 2026
/islamicftz
Shawwal 12 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 577
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

Fitch yaipa Tanzania daraja la B+ uchumi imara

Zanzibar yaja na mkakati wa 'Halal Tourism' kukuza utalii

TAHARIRI: Elimu, hamasa vinahitajika kuchochea uwekezaji H alal

Mwinyi anadi fursa za uwekezaji sekta ya anga

Vita Iran yatishia mtiririko wa mitaji Afrika toka nchi za Ghuba

Kagame aahidi kufufua mradi wa dola milioni 4 wa Waislamu uliyokwama

فتاوى

SHEIKH
Shaaban Mussa

Milioni 43 walitembelea Misikiti Miwili Mitukufu siku 10 za mwanzo za Ramadhan

Hasira zatanda baada ya Msikiti Al-Aqsa kufungwa wiki nne mfululizo

شَوَّال

HABARI ZANZIBAR

NA MWANDISHI WETU

Zanzibar yaja na mkakati wa 'Halal Tourism' kukuza utalii

Katika juhudi za kuimarisha sekta ya utalii visiwani Zanzibar, mamlaka zinazohusika na sekta hiyo zimeanzisha mpango mpya wa kusukuma mbele ajenda ya Utalii Halal unaotajwa kuwa na mafungamano na historia ya kidini.

Mpango huo unalenga kuwavutia watalii kutembelea visiwa hivyo ili kujionea maeneo yenye kukumbusha matukio na historia ya dini.

Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Arif Abbas, amesema Zanzibar inakusudia kuufikisha mbali zaidi Utalii Halal, kwa kuwa mambo yanayofungamana na historia na ustaarabu wa kidini visiwani humo bado yapo.

"Naunga mkono wazo hili na sasa hivi napenda kuishukuru serikali kwa kuwa imeweza kuona fursa kwenye suala hili la halal tourism..., tunaona watu wengi sana wanaenda miji kama Vatican, Jerusalem, lakini pia hapa Zanzibar tuna vivutio vingi sana ambavyo vina michepuko inayotokana na dini," aliongeza Abbas.

Amesema licha ya aina hiyo ya utalii kuwa mpya visiwani Zanzibar, hiyo haimaanishi safari ya kuelekea kilele cha mafanikio itaishia njiani.

Kwa mujibu wa Abbas, hivi sasa Serikali ya Zanzibar inatangaza zaidi Utalii Halal, ikitarajia kuwa katika siku za usoni itakuwa kinara katika sekta hiyo.

Katika mwezi Mtukufu wa Ramadhan uliomalizika hivi karibuni, zaidi ya watu 15,000 walikusanyika katika uwanja wa New Amaan Complex kwa ajili ya kushiriki futari ya pamoja.

Tukio hilo la kufuturisha linatajwa kuvunja rekodi iliyowekwa hapo awali nchini Ethiopia, ambako watu 7,000 walikusanyika pamoja kwa ajili ya futari.

Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi, alilitaja tukio hilo kuwa la aina yake, akisema ni kichocheo kinachosukuma mbele ajenda ya kuimarisha amani, ambayo ndani yake hukuza utalii ukiwamo Utalii Halal.

Kwa mujibu wa takwimu za mamlaka zinazohusika na utalii visiwani Zanzibar, katika mwaka 2025 pekee Zanzibar ilipokea zaidi ya watalii 900,000. Idadi hiyo inatarajiwa kuongezeka katika miaka ijayo kutokana na mipango madhubuti inayolenga kuboresha na kupanua miundombinu ya usafiri.

شَوَّال

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

Fitch Ratings yaipa Tanzania darajala B+ uchumi imara

Tanzania imeendelea kushikilia daraja lake la mikopo la B+ lenye mtazamo thabiti, ikiashiria uchumi unaokua kwa kasi ya wastani na deni linalodhibitika, ingawa bado unakabiliwa na changamoto za kimuundo zinazozuia kasi kubwa ya maendeleo, wachambuzi wanasema.

Shirika la tathmini la Fitch Ratings Ijumaa lilithibitisha daraja la Tanzania la muda mrefu la fedha za kigeni (LTFC) katika kiwango cha "B+" huku mtazamo ukiwa thabiti.

Tathmini hiyo inaonyesha uwiano kati ya mageuzi yanayoendelea na udhaifu uliopo, hali inayodokeza kuwa nafasi ya mikopo ya nchi haitabadilika kwa kiasi kikubwa katika muda mfupi bila mageuzi ya kina zaidi.

Daraja la Tanzania linaakisi ukuaji mzuri wa pato la taifa (GDP) na mfumuko mdogo wa bei, vikichangiwa na mageuzi na upatikanaji wa fedha za nje kupitia mpango wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Hata hivyo, linakabiliwa na changamoto za utawala dhaifu, mapato ya serikali yaliyo chini ikilinganishwa na nchi rika, pamoja na sera za uchumi zisizo imara zinazosababisha changamoto katika soko la fedha za kigeni.

Kwa mujibu wa makadirio ya Fitch, uchumi wa Tanzania unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia sita mwaka 2026 na 2027, ukizidi mataifa mengi yaliyo katika kundi hilo hilo la daraja. Ukuaji huo unatarajiwa kuchochewa na sekta za kilimo, madini na uwekezaji mkubwa katika miundombinu, ikiwemo Reli ya Kisasa (SGR) na Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki katika viwango vya chini, hali itakayosaidia uthabiti wa uchumi.

Kwa upande wa fedha za serikali, bajeti inatarajiwa kuwa na nakisi ya wastani ya takribani asilimia tatu ya GDP, huku deni la taifa likitarajiwa kushuka taratibu kutoka karibu asilimia 50 hadi asilimia 47 ya GDP katika kipindi cha kati.

Ukusanyaji wa mapato umeonyesha kuimarika, ingawa bado uko chini ikilinganishwa na nchi rika. Licha ya mafanikio hayo, wachambuzi wanasema kiwango kidogo cha mapato ya ndani kinaendelea kuizuia Tanzania kujitegemea kikamilifu katika kugharamia maendeleo, hivyo kuongeza utegemezi wa mikopo na misaada ya nje.

Aidha, masuala ya utawala, ufanisi wa taasisi na uthabiti wa sera yanaendelea kuwa muhimu katika kuathiri imani ya wawekezaji.

Akiba ya fedha za kigeni — inayotosha kufidia uagizaji wa bidhaa kwa takribani miezi miwili na nusu — pia inaiacha nchi katika hatari ya misukosuko ya nje, ikiwemo kupanda kwa bei za mafuta na mbolea duniani au mabadiliko katika sekta ya utalii.

NA MWANDISHI WETU

Mwinyi anadi fursa za uwekezaji sekta ya anga

Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali yake itaendelea kuimarisha sekta ya usafiri wa anga pamoja na kuendeleza mageuzi ya kidijitali ili kuvutia uwekezaji na kukuza uchumi.

Dkt. Mwinyi ameyasema hayo Ikulu mjini Zanzibar alipokutana na uongozi wa Liaoning Fangda Group of Companies kutoka China, ulioongozwa na Mwenyekiti wake, Ao Xinhua.

Katika mkutano huo, Rais Dkt. Mwinyi amepongeza dhamira ya kampuni hiyo kushirikiana na Zanzibar katika sekta mbalimbali za uwekezaji na kuahidi ushirikiano wa karibu.

Amesema Zanzibar ina fursa kubwa katika sekta ya anga kutokana na nafasi yake ya utalii, hivyo amewahimiza wawekezaji kutumia fursa hizo kuwekeza katika miundombinu na huduma za usafiri wa anga.

Wanufaika 34 Samia Scholarship wapunguziwa ada ya masomo

Vijana 34 ambao ni wanufaika wa mpango wa Samia Scholarship Extended DS/AI+ watapata punguzo la asilimia 50 ya ada ya masomo katika Chuo cha Limerick nchini Ireland, kufuatia makubaliano yaliyofanywa kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na chuo hicho.

Makubaliano hayo yanalenga kutoa fursa kwa vijana kusoma fani za kisasa, ikiwemo Sayansi ya Data, Akili Mnemba, na Sayansi Shirikishi. Wanafunzi hao ni sehemu ya wanufaika 50 wa mpango unaolenga kukuza ujuzi katika teknolojia za kisasa.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema mpango huo unalenga kuwawezesha vijana wenye vipaji kupata maarifa na ujuzi wa kisasa katika teknolojia, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, inayosisitiza elimu ya sayansi na teknolojia.

Kwa upande wake, Balozi wa Ireland hapa nchini, Nicola Brennan, aliipongeza Serikali kwa kuanzisha mpango huo, akibainisha kwamba utawezesha vijana kurejea nchini wakiwa na ujuzi na uzoefu utakaosaidia kukuza sekta za teknolojia na ubunifu.

شوّال

KALAMU HURU

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Tuache mazoea ya kuingia msikitini bila kuondoa mlio wa simu au kuizima

Kweli inaingia akilini muziki kupigwa msikitini tena ndani ya swala? Swali hili lilikuwa la kushangaza sana kama lingeulizwa miaka 20 au 25 iliyopita, kiasi kwamba mtu angeweza kuliona kama jambo lisilowezekana.
Lakini katika zama hizi za maendeleo ya mawasiliano na simu za kiganjani, jambo hili limekuwa la kawaida na la kusikitisha: Miito ya simu ikiwemo miziki ya 'rusha roho', au nyimbo mbalimbali husikika ndani ya nyumba ya Allah wakati wa ibada ya swala.

Msikiti, mahali tulivu kwa ibada

Msikiti ni sehemu ya utulivu, unyenyekevu na mawasiliano ya moja kwa moja kati ya mja na Mola wake Mlezi. Ni mahali ambapo mioyo inatakiwa itulie, macho yainame na nafsi ijishushe mbele ya Allah.

Lakini inapotokea simu ya mtu inalia kwa sauti ya muziki wakati wa swala, inavunja kabisa hali ya khushuu (unyenyekevu wa ndani ya ibada), si kwa mwenye simu pekee bali hata kwa Waumini wengine walioko msikitini.

Kwa hakika, hali hii inahitaji kukemewa kwa uwazi. Watu wanaoacha simu zao zikiendelea kuita ndani ya swala, bila kuzima au kutoa mlio wanaonesha uzembe wa hali ya juu katika adabu za ibada. Jambo la kusikitisha mtu anaacha simu iendelee kuita kwa muda mrefu, akiwatesa wengine kwa kelele zisizofaa katika nyumba ya ibada.

Huku si tu kukosa adabu kwa watu, bali pia ni kupuuzia heshima ya Allah na sehemu yake ya ibada.

Wengine hujaribu kujitetea kwa kusema kuwa kuzima simu pale inapoita wakati wa swala, kunaweza kuharibu swala zao au kuwasahaulisha nia ya ibada. Huu ni udhaifu wa fikra usio na msingi wa kiakili wala kidini. Kwa kweli, je ni ipi kubwa zaidi: kuhifadhi 'nadharia ya simu isiyokatika' au kuhifadhi heshima ya swala na unyenyekevu wa waumini wote?

Mwenyezi Mungu anasema: "Mna nini hamuogopi adhama ya Allah na hamumpi heshima inayostahiki?" [Qur'an, 71:13]. Aya hii inatukumbusha umuhimu wa kumtukuza Allah katika kila hali, hasa tunapokuwa ndani ya ibada.

Tahadhari kabla ya kuingia msikitini

Tukumbuke kwamba msikiti si mahali pa mazoea ya kidunia kuingilia ibada. Ni mahali pa kuachana na kelele zote za dunia na kuingia katika mawasiliano ya kiroho.

Hivyo basi, kuingia msikitini ukiwa na simu yenye mlio wa muziki ni kosa la kimaadili, kiutamaduni na kiibada. Heshima ya msikiti inahitaji kila Muumini kuchukua tahadhari kabla hata ya kuingia: kuhakikisha simu imetolewa mlio au kuzimwa kabisa.

Zaidi ya hilo, tunapaswa kuelewa kuwa adabu za ibada ni sehemu ya ukamilifu wa imani. Mtu mwenye adabu katika ibada anajijengea mazingira ya khushuu na kumfanya mwingine pia afaidike na utulivu huo. Lakini mtu asiyejali anakuwa chanzo cha usumbufu wa kiroho kwa wengine wote.

Kwa hiyo, ni wajibu wa kila Muislamu anayehudhuria msikitini kuhakikisha kwamba simu yake haileti kero. Ni kitendo rahisi sana: kabla ya kuingia msikitini, zima simu yako au iweke katika hali ya ukimya. Hili si jambo la gharama, bali ni ishara ya heshima, adabu na upendo kwa ibada ya swala na kwa waumini wenzako.

Kwa kumalizia, tukumbuke kwamba maendeleo ya teknolojia hayapaswi kuharibu adabu zetu za kidini. Badala yake, yatufanye tuwe watu wenye nidhamu zaidi. Msikiti unabaki kuwa nyumba ya Allah, na kila mmoja wetu ana wajibu wa kuulinda utukufu wake.

KUTOKA KWA MAJIRANI

MAHMOUD NYAMGUMA

Kagame aahidi kufufua mradi wa dola milioni 4 wa Waislamu uliyokwama

Vyanzo vya ndani vinaeleza kuwa mradi huo unaweza kuongeza ajira kwa zaidi ya watu 2,000 na kuchochea sekta ya utalii wa kidini kwa zaidi ya asilimia 15

Rais wa Rwanda, Paul Kagame ameahidi kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyokwama kwa jamii ya Waislamu nchini Rwanda, ikiwemo ujenzi wa jengo la kisasa la Kiislamu lenye thamani ya zaidi ya faranga za Rwanda bilioni 5 (sawa na takribani dola milioni 4).

Kwa mujibu wa The New Times, Kagame alitoa kauli hiyo alipokutana na jamii ya Kiislamu kuadhimisha Idd al-Fitr jijini Kigali, Kagame amesema serikali itasimamia moja kwa moja utekelezaji wa miradi hiyo ili kuhakikisha Waislamu wanapata maendeleo stahiki kwa wakati.

Waislamu Rwanda wanakadiriwa kufikia asilimia 5 hadi 10, huku ripoti za kimataifa zikibainisha kuwa uhuru wa kuabudu umeimarika kwa zaidi ya asilimia 80 katika muongo mmoja uliopita.

Kagame amesisitiza kuwa maendeleo jumuishi hayawezi kufikiwa bila ushiriki wa makundi yote ya kijamii, akibainisha kuwa historia ya Waislamu nchini humo ni sehemu ya mshikamano wa kitaifa, hasa baada ya mauaji ya halaiki ya 1994.

Mradi huo mkubwa unatarajiwa kujumuisha msikiti wa kitaifa, hospitali ya kisasa, hoteli, majengo ya biashara pamoja na miundombinu ya michezo na burudani.

Vyanzo vya ndani vinaeleza kuwa mradi huo unaweza kuongeza ajira kwa zaidi ya watu 2,000 na kuchochea sekta ya utalii wa kidini kwa zaidi ya asilimia 15 ndani ya miaka mitano ijayo, jambo linaloonekana kuimarisha nafasi ya Waislamu katika uchumi wa taifa hilo.

Akizungumza kwa niaba ya jamii ya Waislamu, Mufti wa Rwanda Sheikh Musa Sindayigaya ameeleza kuridhishwa na hatua zinazochukuliwa na serikali, akitaja mafanikio kama kurahisishwa kwa safari za hija kupitia RwandAir na kuongezeka kwa uwakilishi wa Waislamu serikalini.

شوّال

HABARI
MASHARIKI YA KATI

MAHMOUD NYAMGUMA

Milioni 43 walitembelea Misikiti Miwili Mitukufu siku 10 za mwanzo za Ramadhan

■ **Kwa mujibu wa taarifa nyingine ya SPA, zaidi ya milo 9,015,322 ya futari iligawiwa bure kwa waumini katika Masjid an-Nabawi wakati wa Ramadhan.**



Waumini 43,840,961 walitembelea Misikiti Miwili Mitukufu ya Makkah na Madinah katika siku 10 za mwanzo za mwezi mtukufu wa Ramadhan 1447 Hijria, hali inayoonyesha ongezeko kubwa la mahujaji na waabudu wanaofika katika maeneo hayo matakatifu.

Kwa mujibu wa Saudi Press Agency (SPA), Msikiti Mkuu wa Makkah (Masjid al-Haram) ulipokea waabudu 23,839,592 waliotekeleza swala tano za kila siku pamoja na Taraweeh, huku Waumini 8,110,498 wakifanya ibada ya Umrah.

Kwa upande wa Masjid an-Nabawi mjini Madinah, jumla ya waumini 10,789,467 walitekeleza swala tano na Taraweeh katika msikiti huo. Aidha, waumini 317,025 walipata fursa ya kuswali katika Rawdah Al-Sharifah, huku wageni 784,379 wakitoa salamu kwa Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) pamoja na maswahaba wake wawili.

Kwa mujibu wa taarifa nyingine ya SPA, zaidi ya milo 9,015,322 ya futari iligawiwa bure kwa waumini katika Masjid an-Nabawi wakati wa Ramadhan. Chakula hicho kiligawiwa kila siku kabla ya swala ya Magharibi kupitia mfumo uliosimamiwa na wafanyakazi na wajitolea ili kuhakikisha waumini wanapata mazingira bora ya kufuturu na kuendelea na ibada.

NA MWANDISHI WETU

Saudi Arabia yatoa fursa adhimu kwa waliokwama kuondoka

Saudi Arabia imetoa fursa maalum kwa wageni na wasafiri waliokwama nchini humo ambao visa zao zimekwisha muda, ikiwa ni hatua ya kusaidia watu walioathiriwa na changamoto za usafiri katika eneo la Mashariki ya Kati.

Kwa mujibu wa Saudi Gazette, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Saudi Arabia imeruhusu wenye visa zilizokwisha muda kuweza kuondoka nchini moja kwa moja bila kutozwa faini, au kuomba kuongeza muda wa visa hadi Aprili 18, 2026.

Hatua hiyo inahusu aina mbalimbali za visa, ikiwemo visa za ziara, visa za Umrah, visa za transit pamoja na visa za kutoka nchini (final exit visas) ambazo zilikwisha muda kuanzia Februari 25, 2026.

Kwa mujibu wa mamlaka za Saudi Arabia, wageni wanaotaka kubaki nchini kwa muda zaidi wanatakiwa kuomba kuongeza muda wa visa kupitia mfumo wa Absher na kulipa ada zinazohitajika. Hata hivyo, wale wanaochagua kuondoka moja kwa moja hawatalazimika kulipa faini za kuchelewa.

MAHMOUD NYAMGUMA

Hasira zatanda baada ya Al-Aqsa kufungwa wiki nne mfululizo

Msikiti huo, unaochukuliwa kuwa wa tatu kwa utakatifu katika Uislamu, umefungwa tangu mwishoni mwa Februari kufuatia kile kinachoelezwa kama hatua za dharura zinazohusishwa na vita vinavyoendelea kati ya Israel, marekani na Iran.

Mamlaka za Israel zimeendelea kuwazuia Waislamu kuswali swala ya Ijumaa katika Msikiti wa Al-Aqsa kwa wiki ya nne mfululizo sasa, hatua inayozua taharuki na malalamiko makubwa miongoni mwa waumini, tovuti ya Middle East Monitor inaripoti.

Msikiti huo, unaochukuliwa kuwa wa tatu kwa utakatifu katika Uislamu, umefungwa tangu mwishoni mwa Februari kufuatia kile kinachoelezwa kama hatua za dharura zinazohusishwa na vita vinavyoendelea kati ya Israel, marekani na Iran.

Taarifa za mashuhuda zinaeleza kuwa vikosi vya polisi wa Israel vimeimarisha ulinzi katika eneo la Mji wa Kale wa Jerusalem, vikifunga milango ya kuingia Al-Aqsa na kuwazuia waumini hata kuswali katika maeneo ya karibu kama vile Barabara ya Salah al-Din.

Wakati huo huo, ibada zimeruhusiwa kwa idadi ndogo tu ya walinzi na maafisa wa Waqf ya Kiislamu wanaosimamia eneo hilo. Hatua hiyo imewalazimu Waislamu wengi kuswali katika misikiti midogo midogo ndani ya jiji hilo.

Takwimu za taasisi za Kiislamu zinaonesha kuwa zaidi ya waumini 50,000 hukusanyika katika swala za Ijumaa ndani ya Al-Aqsa katika nyakati za kawaida, hali inayodhihirisha ukubwa wa athari za zuio hilo.

Kufungwa kwa ibada za Idd al-Fitr mwaka huu kunatajwa kuwa tukio la kwanza tangu mwaka 1967, jambo linaloibua maswali kuhusu uhuru wa kuabudu katika eneo hilo lenye mgogoro.

Ripoti mbalimbali za kimataifa, zikiwemo za mashirika ya haki za binadamu, zimeeleza kuwa vizuizi hivyo vinaweza kuongeza mvutano wa kidini na kisiasa katika eneo la Mashariki ya Kati.

Licha ya ukosoaji mkali kutoka mataifa ya Kiislamu na Kiarabu, mamlaka za Israel zimeendelea kushikilia msimamo wao wa kutofungua msikiti huo, zikieleza sababu za kiusalama.

Hata hivyo, wachambuzi wa siasa za eneo hilo wanaona hatua hiyo kama yenye mwelekeo wa kisiasa zaidi kuliko kiusalama.

UKHTI FATIMA SS

Standard Bank yatangazwa benki bora ya Kiislamu tena

Benki ya Standard Bank Shari'ah Banking imetangazwa tena kuwa Benki Bora ya Kiislamu katika tuzo za kimataifa za Global Banking & Finance Review Awards, ikiimarisha nafasi yake katika sekta ya fedha za Kiislamu.

Kwa mujibu wa shirika la habari la News24, hii ni mara ya pili kwa benki hiyo kushinda tuzo hiyo baada ya pia kuibuka mshindi mwaka 2025.

Tuzo hizo hutolewa kwa taasisi za kifedha zinazoonyesha ubunifu, uadilifu na utoaji wa huduma za kifedha zinazofuata kanuni za Sharia. Taasisi zinazoshinda hutathminiwa kwa vigezo kama ubunifu katika bidhaa za kifedha, uwazi wa huduma na mchango wake katika kukuza huduma jumuishi za fedha.

Akizungumzia mafanikio hayo, Mkuu wa Shari'ah Banking wa Standard Bank, Ameen Hassen, alisema ushindi huo unaonyesha kwamba benki hiyo inaendelea kutoa huduma za kifedha zinazofuata misingi ya Kiislamu na kukidhi mahitaji ya wateja.

Uzbekistan nao mbioni kuanzisha Benki za Kiislamu

Zaidi ya benki 10 za kibiashara nchini humo tayari zimeanza maandalizi ya kutoa huduma za kifedha zinazofuata kanuni za Sharia kama murabaha, mudaraba na ijara, jarida la UzDaily linaripoti.

Hatua hiyo ilijadiliwa Machi 25 wakati Rais wa Uzbekistan Shavkat Mirziyoyev alipowasilishiwa mpango wa kuanzisha bidhaa za kifedha za Kiislamu ndani ya mfumo wa benki.

Mpango huo unajumuisha kuanzishwa kwa Baraza la Fedha za Kiislamu chini ya Benki Kuu ili kusimamia viwango na kufuatilia utekelezaji wa kanuni za Sharia katika taasisi za fedha.

Wakati huo huo, jarida la Times of Central Asia linaripoti kuwa mageuzi ya sekta ya fedha ni sehemu ya mkakati mpana wa maendeleo unaolenga kuvutia hadi dola bilioni 50 za uwekezaji mpya nchini humo.

Pakistan mfano wa kuigwa ukuaji mifuko ya uwekezaji halal

Sekta ya uwekezaji wa mifuko inayofuata kanuni za Sharia nchini Pakistan imefikia hatua mpya baada ya thamani ya mali zinazodhibitiwa na mifuko hiyo kuvuka rupia trilioni 2 (zaidi ya USD bilioni 7 kwa mara ya kwanza.

Vyanzo mbalimbali vinaripoti kuwa mali zinazodhibitiwa na mifuko hiyo zilifikia takribani rupia trilioni 2.1 kufikia Februari 2026, kutoka rupia trilioni 1.7 katika kipindi kama hicho mwaka uliopita.

Takwimu hizo zimetolewa na Mutual Funds Association of Pakistan (MUFAP) na zinaonyesha ukuaji wa takribani asilimia 23 kwa mwaka, jambo linaloashiria kuongezeka kwa imani ya wawekezaji katika bidhaa za uwekezaji zinazofuata kanuni za Kiislamu.

Mifuko ya uwekezaji ya Sharia nchini humo inajumuisha aina mbalimbali za bidhaa kama mifuko ya fedha za soko la fedha, mifuko ya hisa, mifuko ya mapato pamoja na mifuko ya pensheni ya Kiislamu. Uwekezaji huo huwekwa katika hisa, sukuk na vyombo vingine vinavyokubalika kwa mujibu wa Sharia.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa kampuni ya Al Meezan Investment Management inaongoza sekta hiyo kwa kusimamia mali yenye thamani ya zaidi ya rupia bilioni 701.

شوّال

HABARI
MOROGORO

NA YUSUFU AMINI

Waziri aelekeza hatua kali kwa tiba asili zisizosajiliwa

■ Amesema hatua hiyo inalenga kupunguza vifo na madhara ya kiafya yanayosababishwa na matumizi ya dawa bila mwongozo sahihi wa kitaalamu.

Waziri wa Afya, Bw. Mohamed Mchengerwa, ameagiza msako mkali dhidi ya madaktari na waganga wa jadi wasiosajiliwa, akisisitiza kuwa watu wote wanaotoa huduma za tiba au dawa za asili lazima wasajiliwe rasmi.

Amesema hatua hiyo inalenga kupunguza vifo na madhara ya kiafya yanayosababishwa na matumizi ya dawa bila mwongozo sahihi wa kitaalamu.

Bw. Mchengerwa alitoa agizo hilo Jumatano, Machi 25, 2026, alipokuwa akitembelea banda la Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) wakati wa mkutano na waganga wa tiba asili jijini Dodoma.

Alisisitiza kuwa watoa huduma wote wanapaswa kutambuliwa kupitia usajili chini ya vyombo husika vinavyosimamia utafiti na huduma za tiba asili.

"Si sahihi kwa taifa kuruhusu mtu yeyote kujitangaza kuwa daktari au mganga wa jadi bila kutambuliwa. Kama mtu anatoa ushauri wa kitabibu, ni lazima tujue yeye ni nani na kama ameidhinishwa," alisema.

Kauli hiyo imekuja wakati kukiwa na ongezeko kubwa la maduka ya dawa za asili katika miji mikubwa, hali inayozua hofu kuhusu udhibiti wa sekta hiyo.

Licha ya kupanuka kwa huduma za matibabu ya kibingwa nchini, ikiwemo tiba ya saratani, upandikizaji figo, upasuaji wa moyo, upasuaji wa ubongo, upandikizaji uboho na huduma za uzazi kwa njia ya maabara (IVF), matumizi ya dawa za asili nayo yamekuwa yakiongezeka.

Katika eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam, mtaa ambao hapo awali ulikuwa na maduka ya kawaida sasa una maduka mengi ya dawa za mitishamba. Hali kama hiyo pia inaripotiwa katika maeneo ya Mbagala, Buguruni na Manzese, ambako dawa za asili, za ndani na zinazoagizwa kutoka nje, zimeenea kwa kasi.

Wafanyabiashara wa Kariakoo wanasema kodi ya pango kwa kibanda kimoja huanzia Sh800,000 hadi zaidi ya Sh2 milioni kwa mwezi, ishara kuwa biashara hiyo inaendelea kuwa na faida licha ya gharama kubwa.

Bw. Mchengerwa alionya kuwa baadhi ya watoa huduma huwazuia wagonjwa kwenda hospitalini na badala yake kuwashauri kutumia dawa zisizothibitishwa, jambo alilosema limechangia matatizo makubwa ya kiafya.

"Tunaona vijana wengi wenye umri wa miaka 15, 16 na 17 wakipata matatizo ya figo kutokana na kutofuata taratibu sahihi," alisema.

Aliielekeza NIMR kuhakikisha kuwa mtu yeyote anayedai kuwa na dawa ya kutibu ugonjwa lazima asajiliwe na kuthibitishwa, akionya kuwa watakaokaidi watachukuliwa hatua za kisheria.

"Maelekezo yangu ni kuweka mfumo madhubuti wa kuwatambua waganga wote wa tiba asili. Serikali itawalinda wanaofuata sheria, lakini yeyote anayezungumzia dawa lazima apitie mfumo unaotambuliwa na dawa zake ziidhinishwe," alisema.

Aidha, aliiagiza taasisi hiyo kutoa taarifa kwa umma kuhusu dawa za asili zilizoidhinishwa na kuiagiza wizara kusaidia programu za mafunzo kwa wataalamu ili kuboresha viwango vya huduma.

Akizungumza katika mkutano huo, Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Grace Magembe, alisema tiba asili hutumiwa na takribani asilimia 60 ya Watanzania, huku duniani ikitumika na karibu asilimia 80 ya watu.

Aliongeza kuwa ukaguzi uliofanywa mwaka jana ulibaini kuwa asilimia 17 ya dawa za asili zilichanganywa na vitu visivyofaa, huku asilimia 25 zikiwa zimeathiriwa na uchafuzi kutokana na uhifadhi duni, hali iliyosababisha kuchukuliwa hatua kwa wahusika.

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 1

Na Said Rajab

0783 650 803

VITA YA MAREKANI NA IRAN:

Vitisho vya Trump na yaliyojificha nyuma ya pazia

Wakati Marekani na 'kikaragosi' chake, Israel walipoanzisha vita ya uchokozi dhidi ya Iran mnamo Februari 28, 2026, waliweka muda wa vita hiyo kuwa siku nne.

Vitisho vya Trump na yaliyojificha nyuma ya pazia

Wakati Marekani na 'kikaragosi' chake, Israel walipoanzisha vita ya uchokozi dhidi ya Iran mnamo Februari 28, 2026, waliweka muda wa vita hiyo kuwa siku nne.

Waliamini kwamba mara tu Kiongozi Mkuu wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei atakaposhambuliwa na kuuawa, kiongozi atakayefuata angejisalimisha na kukubali masharti yao kama ilivyotokea Venezuela wakati Rais wake alipotekwa, na Naibu wake kujisalimisha kwa Marekani.

Hata hivyo, hali haikuwa kama walivyotarajia. Iran ilibaki imara na kukabiliana vilivyo na mashambulizi ya Marekani na Israel. Kiburi cha Rais Donald Trump kiliongezeka zaidi, hata kufikia hatua ya kutangaza kwamba angeshiriki kumteua Kiongozi Mkuu mpya wa Iran, huku akisisitiza kuwa hataki mtoto wa Khamenei achukue nafasi hiyo. Hata hivyo, matumaini hayo yalipotea.

Gazeti la New York Times liliripoti, likinukuu vyanzo vya kuaminika mnamo Machi 12, 2026 kwamba, washauri wa Trump waliendelea kuamini kuwa kuangamiza watawala wakuu wa Iran kungeibua viongozi wengine ambao wangeweza kukomesha vita.

Kauli hiyo pia iliungwa mkono na Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Pete Hegseth mnamo Machi 10, 2026, aliposema: "Siwezi kusema kwamba tulitarajia kuwa hivyo ndivyo watakavyoitikia."

Baada ya siku nne kupita, Trump alidai kuwa angemaliza vita hiyo ndani ya wiki mbili, au pengine wiki nne. Lengo lake lilikuwa kumaliza vita hiyo kabla haijawa mbaya zaidi na kuathiri nchi yake, hasa ikizingatiwa kuwa uchaguzi wa katikati ya muhula wa Bunge la Congress umepangwa kufanyika Novemba 3, 2026.

Katika siasa, kuchukulia mfano wa jumla ni kosa, kwa kuwa kila tukio lina mazingira na muktadha wake. Vivyo hivyo, kuondoa tukio katika muktadha wake maalumu ni upotoshaji wa hali halisi.

Hata hivyo, kiburi na ufedhuli vimempofua macho Donald Trump, kama ilivyowahi kutokea kwa mtangulizi wake wa Republican, George .W. Bush, aliposhambulia Afghanistan mwaka 2001 na Iraq mwaka 2003, na pia George H. W. Bush wakati wa uvamizi wa Somalia mwaka 1992.

Marekani na washirika wake hutegemea nguvu zao za kijeshi na kiuchumi, pamoja na ukimya wa mataifa mengine. Kwa msingi huo, hushughulikia kila nchi kivyake bila kukabiliwa na nguvu kubwa ya upinzani.

Hali ilikuwa tofauti wakati wa dola ya Muungano wa Kisovieti (USSR), ambapo Marekani ililazimika kuzingatia nguvu ya kambi ya kikomunisti na kutafuta makubaliano nayo kuanzia mwaka 1961 hadi 1991, iliposambaratika na kuiacha Marekani ikiwa nguvu kuu pekee duniani.

Hivi sasa, wakati vita ya Marekani na Israel dhidi ya Iran ikiingia wiki yake ya nne, Donald Trump ameanza kulegeza msimamo wake wa awali, akidai aidha amefanikisha malengo yake au akionesha nia ya kusitisha vita.

Malengo hayo ni pamoja na kuizuia Iran kupata silaha za nyuklia, kuizuia kutengeneza makombora ya masafa marefu, na kuwahamasisha wananchi wa Iran kuupindua utawala wao na kuweka uongozi utakaoitii Marekani na Israel.

Katika kukabiliana na mashambulizi ya Marekani na Israel, Iran ilijibu mapigo kwa kulenga maslahi ya Marekani katika eneo la Mashariki ya Kati na Ghuba ya Uajemi na kushambulia vituo vya mafuta katika mataifa ya Ghuba, jambo lililoathiri uzalishaji wa mafuta na kusababisha kufungwa kwa Mlango-Bahari wa Hormuz, ambako hupitia takriban asilimia 20 ya usambazaji wa nishati duniani.

Matokeo yake, mgogoro wa mafuta umeibuka duniani kote, usambazaji umepungua na bei kupanda kwa kasi, kuanzia Marekani hadi masoko ya kimataifa.

Hata utolewaji wa akiba ya kimkakati haukutosha kupunguza bei, ambazo zimeendelea kupanda huku Iran ikiongeza mashambulizi yake katika miundombinu ya mafuta ya eneo hilo.

Kutokana na hali hiyo, Trump alianza kutoa kauli zinazokinzana. Machi 11, 2026 aliliambia shirika la habari la Axios katika mahojiano ya simu kuwa vita hiyo itaisha hivi karibuni, akidai kuwa hakukuwa na shabaha muhimu iliyobaki Iran.

Trump alinukuliwa akisema: "Wakati wowote nitakapotaka vita itaisha." Kauli hiyo ilionekana kama ishara ya kutaka kumaliza mzozo huo.

Aidha, Trump alionesha kuchanganyikiwa kuhusu athari za vita katika usambazaji wa mafuta, alipomwambia Brian Kilmeade wa Fox News kuwa meli zinazozuiwa kupita Mlango – Bahari wa Hormuz zinapaswa kuonesha ujasiri na kulazimisha kupita.

Kwa tafsiri nyingine, Trump aliwataka washirika wake wahatarishe maisha yao kwa maslahi ya Marekani – lakini hakuna aliyeonesha utayari huo. Machi 14, 2026, Trump alilazimika kutoa wito kwa mataifa mengine kusaidia kufungua tena Mlango – Bahari wa Hormuz.

Itaendelea katika toleo lijalo, Insha Allah

شوّال

فتاوى

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Swali: Ni ipi hukumu ya bima ya afya ikiwa hakuna mbadala wa Kiislamu?

Jibu: Bima ya afya ni miongoni mwa masuala mapya (nawazil) yaliyojitokeza katika zama za sasa. Haikujulikana kwa jina hili wala kwa mfumo wake katika zama za mwanzo wa Uislamu. Kwa sababu hiyo, wanazuoni wameichunguza kwa kina ili kubaini hukumu yake kwa kuilinganisha na mikataba inayofanana nayo katika fiqhi ya Kiislamu.

Moja ya shaka zinazotolewa kuhusu bima ya afya ni kuifananisha na bima ya maisha au bima ya kibiashara (commercial insurance). Kwa ujumla wake, aina hii ya bima imehukumiwa kuwa haramu kwa sababu ya kuwepo kwa gharar (kutokujulikana kwa matokeo), riba, na kula mali kwa batili.

Hata hivyo, uchunguzi wa kina unaonesha kuwa bima ya afya inatofautiana na bima ya maisha katika mambo kadhaa muhimu.

Kwanza, bima ya maisha ni mkataba unaojengwa juu ya kutokujulikana (jahala) na gharar kubwa hasa katika kiwango cha fidia na muda wake. Mtu hulipa michango bila kujua kwa uhakika atapata nini na lini. Hali hii inaleta hatari ya kukiuka misingi ya haki katika miamala ya Kiislamu.

Lakini kwa upande wa bima ya afya, mara nyingi mkataba wake unahusu huduma halisi ya matibabu ambayo ipo au inatarajiwa kupatikana. Hapa, mtu halipi kwa matarajio ya kupata fedha nyingi baadaye, bali hulipia huduma ya afya atakayohitaji. Hivyo, kiwango cha gharar kinakuwa kidogo na kinachovumilika katika aina hii ya mkataba.

Pili, bima ya maisha iko katika mikataba ya kubadilishana (mu'awaḍhwaat) inayofanana na biashara au upangaji (ijarah), ambapo sharti ni kuondoa kabisa gharar na dhulma. Kinyume chake, bima ya afya inaweza kuangukia katika mikataba ya kusaidiana au kunufaishana (irtifaq), ambapo kiwango kidogo cha kutokujulikana kinaweza kuvumiliwa.

Wanazuoni wengine wamejaribu pia kuitazama bima ya afya kwa mtazamo wa mkataba wa ju'alah (malipo kwa matokeo). Kwa mfano, katika vitabu vya fiqhi imeelezwa kuwa mtu anaweza kusema: "Yeyote atakayemtibu mgonjwa wangu mpaka apone, atapata kiasi fulani cha fedha." Mkataba huu unaruhusiwa. Hapa malipo yanahusishwa na matokeo (kupona), si juhudi pekee.

Imepokewa pia kauli ya mwanazuoni mashuhuri Ibn Taymiyyah akieleza kuwa inajuzu kumpa tabibu malipo kwa kupona kwa mgonjwa. Ametolea ushahidi kisa cha wale Swahaba wa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) waliomponya kiongozi wa kabila kwa ruqyah wakapewa kondoo, na Mtume akakubali kitendo hicho. Hii inaonesha uhalali wa kulipia matokeo ya matibabu, si lazima huduma yenyewe iwe na uhakika wa matokeo kabla.

Kwa msingi huu, baadhi ya wanazuoni wameona kuwa bima ya afya inaweza kuvumiliwa au kuruhusiwa, hasa inapokuwa haina riba ya wazi na inapolenga kutoa huduma ya matibabu badala ya kuwa chombo cha biashara ya fedha.

Hata hivyo, jambo muhimu la kuzingatia ni hali ya ulazima (ḍharura). Ikiwa hakuna mbadala wa Kiislamu unaopatikana—kama vile bima za ushirika (takaful)—na mtu anahitaji bima ya afya kwa ajili ya kulinda maisha yake au familia yake dhidi ya gharama kubwa za matibabu, basi wanazuoni wengi huruhusu kujiunga nayo kwa kiwango cha haja.

Kwa kumalizia, hukumu ya bima ya afya si sawa na ile ya bima ya maisha. Inatofautiana kwa sababu ya asili ya huduma inayotolewa na namna mikataba yake inavyoundwa. Ikiwa itazingatia misingi ya haki, kuepuka riba, na kuwa na kiwango kidogo cha gharar kinachovumilika, basi inaweza kuruhusiwa hasa pale ambapo hakuna mbadala wa Kiislamu na kuna haja ya kweli ya huduma hiyo.

Katika zama hizi, kampuni za bima zimeenea sana, zikiwemo zile za bima ya afya. Katika baadhi ya nchi na mazingira, bima ya afya imekuwa karibu kuwa lazima kwa mtu binafsi na familia yake, hasa kutokana na gharama kubwa za matibabu na mifumo ya huduma za afya.

Hata hivyo, ukweli uliopo ni kwamba nyingi ya kampuni hizi hazijajengwa kwa kuzingatia misingi ya Sharia. Mikataba yao mara nyingi hujumuisha mambo yenye utata kama riba au gharar kwa viwango vinavyoweza kuwa vikubwa. Hapa ndipo suala la hukumu linapohitaji mizani ya kielimu na kifiqhi.

Ikiwa mtu analazimika kujiunga na bima ya afya—kwa mfano sheria ya nchi inamlazimisha, au hana njia nyingine ya kupata huduma za matibabu isipokuwa kupitia bima—basi hali hii inachukuliwa kuwa ni dharura au haja yenye uzito. Katika mazingira kama haya, hakuna tatizo kujiunga nayo, kwa sababu dharura huruhusu yale ambayo kiasili yangekuwa hayaruhusiwi, kwa kiwango kinachohitajika tu.

Lakini ikiwa kujiunga na bima hiyo ni hiari, si lazima, basi tahadhari zaidi inahitajika. Katika hali hii, mtazamo bora ni kwamba mtu anapaswa kujiepusha kunufaika zaidi ya kiwango alichochangia. Yaani, kama atalipwa fidia au kufidiwa gharama, ajitahidi kuchukua kile kinacholingana na haki yake tu au kiasi alichotoa au kinacholingana na hasara aliyopata, na si kujinufaisha kupita kiasi hata kama mfumo wa kampuni ungemruhusu kufanya hivyo.

Hii inalenga kulinda nafsi ya Muislamu dhidi ya kula mali isiyokuwa ya haki, na kudumisha

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania
Mhariri
+255 789 201383

Elimu, hamasa vinahitajika kuchochea uwekezaji halal

Katika dunia ya sasa, Sukuk (au hati fungani za Kiislamu) imekuwa mbadala muhimu wa uwekezaji katika masoko ya hisa na mitaji duniani. Uwekezaji huu unafanyika kwa mujibu wa sharia za Kiislamu na unatoa fursa kwa mtu binafsi, kampuni au serikali kuwekeza katika miradi mbalimbali kwa kuzingatia usawa, uadilifu na bila kutozwa riba.

Hii ina maana kuwa wawekezaji wanakubali hatari za kibiashara (profit and risk sharing), tofauti na mifumo ya riba inayopokelewa na wadai wa hati fungani zisizo za Kiislamu (Conventional Bonds), ambapo mwekezaji hupewa ahadi ya kurejeshewa fedha zake pamoja na riba (interest), ambayo ni haramu katika Uislamu.

Sukuk inahimiza uwekezaji unaohusishwa na mali halisi au shughuli halali za kiuchumi, na huwapa wawekezaji mapato yanayotokana na faida au mapato ya mradi unaofadhiliwa. Mfumo huu unalenga kuhakikisha haki, usawa na uadilifu kati ya mwekezaji na mtoaji.

Pamoja na faida hizi lukuki, changamoto kubwa inayojitokeza ni uelewa mdogo kwa baadhi ya watu, ambao huichukulia Sukuk kama bidhaa ya kifedha inayowahusu Waislamu pekee. Watu wengi hawafahamu tofauti kati ya Sukuk na hati fungani za kawaida.

Ni muhimu kuelewa kuwa Sukuk si kwa ajili ya watu wa dini fulani pekee, bali inaweza kutumiwa na mtu yeyote anayevutiwa na uwekezaji unaozingatia sharia na kanuni za Kiislamu, uwazi na uthabiti.

Kutokana na umuhimu huo, elimu kwa umma inahitajika ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi na kuondoa dhana potofu kuhusu Sukuk. Bila elimu ya kutosha, Sukuk itabaki kuwa dhana ngeni kwa wengi, hivyo kupunguza ushiriki wao katika soko la mitaji la Kiislamu.

Kwa minajili hiyo basi, ipo haja ya kuwatumia wataalamu wa masuala ya uchumi na fedha wa Kiislamu katika kuhamasisha umma kuhusu uwekezaji halal. Hili linaweza kufanyika kupitia vyombo vya habari, kampeni za uhamasishaji na semina mbalimbali. Masheikh, wanazuoni na wadau wengine, pia wana wajibu wa kuhakikisha elimu hii inawafikia watu wa kada zote kwa upana. Elimu hii si tu itazisaidia kampuni kufanya maamuzi bora ya uwekezaji, bali pia itachochea ushiriki mpana katika maendeleo ya taifa, huku wananchi, bila kujali tofauti ya dini zao wakinufaika kikamilifu na fursa hii adhimu.

Eneo jingine muhimu linaloweza kutumika kutoa elimu kuhusu hati fungani za Kiislamu (Sukuk) ni shuleni, vyuoni na katika taasisi nyingine za elimu. Kwa kufanya hivyo tutaweza kujenga kizazi chenye uelewa mpana wa masuala ya uchumi na fedha wa Kiislamu.

Jambo muhimu na la msingi kwa mashirika yanayojihusisha na utoaji wa hati fungani za Kiislamu, ni kutoa maelezo ya wazi kuhusu jinsi Sukuk zinavyofanya kazi, faida zake na hatari zinazoweza kujitokeza. Aidha, uwazi na uaminifu katika utoaji na usimamizi wa hati fungani hizi ni muhimu ili kujenga imani kwa wananchi na kuvutia wawekezaji zaidi.

Afya
Pure Drinking water
"Afya" is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.
WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com

شوّال

MAKALA MAALUM

Na Said Rajab
0783 650 803

Funzo kutoka mashambulizi ya Marekani dhidi ya Iran

Mashambulizi mazito kutoka angani, ardhini na baharini ya Marekani na Israel dhidi ya shabaha mbalimbali nchini Iran yameacha funzo kubwa kwa nchi zote za Waislamu duniani.

Mashambulizi hayo ya kikatili yamefanywa dhidi ya Iran wakati ambapo nchi hiyo ilikuwa ikizunguka kwenye duara la ushawishi wa Marekani, ikiipa huduma Marekani katika vita vyake dhidi ya Iraq, Afghanistan na maeneo mengine.

Marekani haikuzungumzia suala la makombora na silaha za nyuklia za Iran. Kiukweli, Rais wa zamani wa Marekani, Barack Obama alihitimisha makubaliano ya mwaka 2015 kwa ushiriki wa nchi za Ulaya, ambapo aliiruhusu Iran kurutubisha madini ya urani hadi kufikia asilimia 3.67.

Iran ilibaki ndani ya duara la Marekani kwa wakati huo kama ilivyo Uturuki hivi sasa. Lakini Rais Donald Trump alipoingia madarakani alitaka Iran iwe kibaraka wake, iseme anachosema na kufanya anachotaka.

Awali, Trump aliingia kwenye mazungumzo ya kitapeli ya nyuklia huko Muscat, ambayo yalidumu kwa takriban raundi tano. Kisha yakaja mashambulizi ya Trump na Mazayuni dhidi ya Iran yaliyopewa jina la 'Vita vya Siku 12'.

Trump alitangaza kuvilenga vituo vitatu vya nyuklia vya Iran, akithibitisha mafanikio ya shambulio la Marekani. Alionesha kwamba maeneo ya nyuklia ya Fordow, Natanz na Isfahan yalishambuliwa na kutoa wito kwa Iran kufanya mazungumzo ya amani na kukomesha vita.

Kwa upande wake, Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Pete Hegseth alithibitisha kwamba shambulio hilo la Marekani limeondoa kabisa matarajio ya nyuklia ya Iran (BBC, 22/06/2025).

Hata hivyo, mashambulizi hayo hayakufanikiwa kuifanya Iran ihame kutoka nchi inayozunguka kwenye duara la ushawishi wa Marekani na kuwa dola kibaraka ya Marekani. Badala yake, zinasikika sauti nchini humo, ingawa ni chache, zikitaka Iran ijitenge kutoka kwenye duara la Marekani.

Kwa hiyo, Marekani ilirudi tena kwenye ujanja wa mazungumzo ya kitapeli, ikizingatia masuala yale yale, yaani kupokonya makombora ya Iran na silaha za kinyuklia. Wakati ule, Marekani ilifanya shambulio dhidi ya Iran baada ya raundi tano za mazungumzo, lakini mashambulizi ya kipindi hiki yametokea baada ya raundi tatu!

Ndugu zangu katika imani, watawala katika nchi za Waislamu wameshindwa kuelewa uzito wa kuwa washirika wa makafiri na kwamba jambo hilo huleta fedheha hapa duniani na adhabu kali kesho Akhera: "Wale ambao huwafanya makafiri kuwa ndiyo marafiki badala ya Waumini. Je! Wanataka wapate kwao utukufu? Basi hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu." [Qur'an, 4:139].

Mataifa ya kikafiri, kimsingi yanajali zaidi maslahi yao wenyewe na yana uadui mkubwa na Uislamu na Waislamu, usiku na mchana, kama alivyobainisha Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu hivi karibuni, aliposema: "Vita yetu ni dhidi ya Uislamu, iwe Sunni au Shia."

Ikiwa wanaonesha kuridhika na nchi yoyote inayozunguka kwenye duara lao la ushawishi, basi ni kwa sababu hawaitakii mema nchi hiyo, na ujue kwamba wanaficha uovu wao. Marekani haiwathamini watawala wa nchi za Waislamu kiasi kwamba, iwapo maslahi yao yatahitaji kuwang'oa madarakani basi itawang'oa!

Ni vyema watawala wa nchi za Waislamu wakajifunza kutoka kwenye historia. Watawala wangapi vibaraka, ambao Marekani imewatupa mara tu baada ya kumaliza jukumu lao la kuwatumikia?

Kama wangekuwa makini wangewapuuza makafiri, lakini wao wamegeuka viziwi, mabubu na vipofu, kamwe hawatarejea. Utiifu wao kwa makafiri umefikia hatua ambayo nchi yao yoyote inaposhambuliwa, nyingine haziendi kuisaidia.

Wanachoona bora zaidi kufanya ni kuhesabu watu wanaokufa na wanaojeruhiwa, kama ilivyo katika mashambulizi dhidi ya Iran! Uislamu pekee ndiyo utakaowanusuru Waislamu duniani.

Ama kuhusu Israel, hiki ni kidola kidogo mno kupewa uzito wowote, kwa sababu uhai wake unategemea zaidi Marekani na mataifa ya Magharibi, na kamwe hakiwezi kukabiliana na Waislamu peke yake, kama alivyosema Mwenyezi Mungu: "Hawatakudhuruni ila ni maudhi tu. Na wakipigana nanyi watakupeni mgongo (watakimbia), na tena hawatakuwa na wa kuwasaidia." [Qur'an, 3:111].

MAKALA MAALUM

Na Abeid Othman
0754 990 083

Usirudie makosa uliyofanya Ramadhan hii

Ramadhan ya mwaka 2026 imefika kikomo, lakini hii si hitimisho la ibada zetu bali mwanzo wa safari mpya ya kujitathmini, kujirekebisha na kujiandaa kwa Ramadhan ijayo, kwa wale watakaojaaliwa uhai.

Mwezi huu mtukufu umebeba mafunzo makubwa, na kila mmoja wetu anatakiwa ajiulize: Je, nimebadilika? Je, nimekuwa mchamungu zaidi?

Hakika, Ramadhan siyo tu mwezi wa kujizuia kula na kunywa, bali ni mwezi wa kujenga nafsi, kuisafisha roho, na kumkaribia zaidi Mwenyezi Mungu. Ndiyo maana lengo kuu la funga limeelezwa wazi kuwa ni kufikia uchamungu. Hivyo basi, baada ya kumalizika kwa mwezi huu, ni muhimu kila Muislamu aketi chini na kufanya tathmini ya kina kuhusu mwenendo wake.

Kwanza, jiulize, ulizingatia ibada zako ipasavyo? Swala zako zilikuwa kwa wakati na kwa unyenyekevu? Ulisoma Qur'an kwa kuelewa au ulikuwa unasoma kwa mazoea tu?

Je, ulimkumbuka Mwenyezi Mungu kwa dhikr na dua, au ulirudi katika shughuli zako za kila siku bila kumtilia maanani haya? Maswali haya si ya kukukatisha tamaa, bali ni ya kukusaidia kuona wapi ulifanya vizuri na wapi unahitaji kuboresha.

Pili, angalia mwenendo wako wa kimaadili. Ramadhan hutufundisha subira, uvumilivu, na nidhamu. Je, uliweza kujizuia na hasira? Je, ulimheshimu mwenzako, kusaidia wenye uhitaji, na kuacha maneno mabaya?

Kama bado ulijikuta ukitenda makosa yale yale kama kugombana, kusema uongo, au kufanya dhambi, basi hiyo ni ishara kuwa bado kuna kazi ya kufanya katika kujenga uchamungu wako.

Usikate tamaa

Ni muhimu kufahamu kuwa si kila mtu hufikia kiwango kile kile cha uchamungu katika Ramadhan. Wapo walioweza kubadilika kwa kiasi kikubwa, na wapo ambao bado wanapambana.

Kama wewe ni miongoni mwa wale ambao hawajafikia malengo yao ya kiroho mwaka huu, usikate tamaa bali chukulia hali hiyo kama changamoto ya kujipanga upya.

Ramadhan hii iwe somo kwako. Kila kosa ulilofanya liwe darasa la kukuandaa kwa Ramadhan ijayo. Kama hukuweza kuswali Taraweeh mara kwa mara, anza sasa kujenga mazoea ya kuswali swala za sunnah. Kama hukuweza kusoma Qur'an kwa wingi, anza hata kwa aya chache kila siku. Hii itakusaidia kufika Ramadhan ijayo ukiwa tayari, badala ya kuanza upya kila mwaka bila mabadiliko ya kweli.

Maandalizi ya Ramadhan hayaanzi siku chache kabla ya mwezi huo kuanza. Yanaanza sasa mara tu baada ya Ramadhan kuisha. Ni katika miezi hii mingine ambapo unajijenga, unajifunza, na kujiweka karibu na Mwenyezi Mungu. Ukisubiri hadi Shaaban ndipo uanze kujipanga, mara nyingi utajikuta huna msingi imara wa kiroho.

Pia, jiwekee malengo ya wazi kwa Ramadhan ijayo. Usiruhusu Ramadhan nyingine ipite bila mpango. Andika malengo yako: unataka kusoma Qur'an mara ngapi? Unataka kuongeza ibada gani? Unataka kuacha tabia gani mbaya? Malengo haya yatakupa mwelekeo na kukusaidia kupima maendeleo yako.

Aidha, usisahau umuhimu wa dua. Muombe Mwenyezi Mungu akupe uhai, afya, na uwezo wa kufikia Ramadhan ijayo. Pia muombe akupe nguvu ya kubadilika na kuwa bora zaidi. Bila msaada wa Mwenyezi Mungu, jitihada zetu pekee hazitoshi..

Usirudi nyuma

Ni vyema pia kujenga mazingira yatakayokusaidia kubadilika. Kaa na watu wema watakaokukumbusha mema na kukuhimiza kufanya ibada. Epuka mazingira yanayokurudisha nyuma katika dhambi na uzembe.

Kwa wale waliofanikiwa kufikia kiwango kizuri cha uchamungu katika Ramadhan hii, nao hawapaswi kulegea. Changamoto kubwa huja baada ya Ramadhan, pale mtu anaposhindwa kudumisha yale mazuri aliyojifunza. Endelea na ibada zako, hata kama si kwa kiwango kile kile cha Ramadhan. Muhimu ni kudumisha mwendelezo.

Kumbuka, thamani ya Ramadhan haipo tu katika siku zake 29 au 30, bali ipo katika mabadiliko unayoyafanya katika maisha yako yote.

Kama baada ya Ramadhan unarudi katika maovu yale yale bila hata juhudi ya kubadilika, basi unahitaji kutafakari upya maana ya ibada zako.

Kwa hiyo, usirudie makosa uliyofanya Ramadhan hii. Kama ulipoteza muda mwingi katika mambo yasiyo na faida, jipange vizuri zaidi mwaka ujao. Kama hukuweza kudhibiti nafsi yako, anza sasa kujifunza kujizuia. Kama hukuweza kuwa karibu na Mwenyezi Mungu, tafuta njia ya kumkaribia kila siku.

Ramadhan ya 2026 imeisha, lakini safari ya uchamungu haijaisha. Huu ni mwanzo mpya.

Ni fursa nyingine ya kujenga nafsi bora, moyo safi, na maisha yenye mwelekeo wa kumridhisha Mwenyezi Mungu. Kwa wale watakaojaaliwa uhai, Ramadhan ijayo iwe bora zaidi kuliko hii iliyopita.

شوّال

NASAHA ZA WIKI
0787 503 085

NA YUSUFU AMINI

Ni muhimu kutathmini funga zetu

Kwa hakika, mafanikio ya kweli ya Muislamu huthibiti katika kuendeleza maadili ya dini, nidhamu na uchamungu katika maisha yake ya kila siku, na si wingi wa ibada alizozifanya ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan pekee.

Kama ukweli ndiyo huo, kila mmoja wetu anapaswa ajiulize: Je, Ramadhan imenibadilisha kwa kiwango gan? Na je, nitawezaje kudumisha mabadiliko hayo?

Inajulikana kwamba miongoni mwetu walianza kuacha baadhi ya ibada walizokuwa wakifanya mwanzoni mwa Ramadhan. Wanasahau kuwa matendo mbalimbali ya kiibada waliyoyafanya ndani ya Ramadhan pia wanapaswa kuyafanya katika miezi mingine.

Kushindwa kutekeleza ibada baada ya Ramadhan ni kielelezo cha upungufu na kasoro katika ibada tulizozifanya ndani ya Ramadhan. Sote tuna yakini kwamba maisha yetu hapa duniani ni mafupi, na kwa hakika Allah haicheleweshi nafsi pindi muda wake wa kuondoka unapowadia.

Kwa kuzingatia hilo, yatupasa kutathmini ibada ya funga ya Ramadhan tulioimaliza hivi karibuni. Allah Mtukufu anasema: "Ibada zote ni zake mwanadamu isipokuwa swaumu, kwani hiyo ni yangu, na Mimi ndiye nitakayeilipa." [Bukhari na Muslim].

Allah ameamua hivyo kwa sababu yeye pekee ndiye anayejua uhakika wa mja kama funga yake ni kamilifu, pungufu au imebatilika. Kwa maana hii, kuna waliofaidika na mwezi wa Ramadhan, na pia kuna walioambulia patupu (wamepata hasara).

Miongoni mwa waliofaidika na Ramadhan ni pamoja na waumini ambao, kwa sababu ya kutafuta malipo bora ya Akhera waliweza kutekeleza ibada ya funga na nyinginezo kwa nia thabiti, Ikhlas na imani kamili.

Waumini wa sampuli hii hupatwa na majonzi ya kusikitika pindi Ramadhan inapomalizika, kwani hawajui kama watajaaliwa tena kuifikia Ramadhan nyingine.

Kinyume na hao, wapo waliofunga kwa kujizuia kula na kunywa huku wakifanya ibada muhimu za sala, kutoa sadaka na nyinginezo, lakini hawakujiepusha na madhambi ya usengenyi, kusema uongo, kufitinisha, kutukana na kuwavunjia heshima watu wengine.

Ni katika hali hii, mtu anaweza kufunga swaumu ya Ramadhan lakini asifaidike na funga yake. Abu Huraira (Allah amridhie) alimsikia Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akisema: "Inawezekana mtu anayefunga asipate chochote katika funga yake isipokuwa njaa, na yule anayesimama usiku kusali asipate chochote isipokuwa uchovu." [Ibn Majah].

Hadith hii inathibitisha kuwa ufungaji usioambatana na kujiepusha na mambo maovu na machafu haumpatii mfungaji faida yoyote. Kando na makundi hayo mawili, pia wapo waliofunga mwezi wa Ramadhan ili waonekane wameidiriki ibada ya swaumu.

Kadhalika, kuna waliolazimika kufunga kwa sababu ya mashinikizo ya watu wanaowazunguka au kwa hofu ya kuitwa 'makobe'. Aghlabu watu wa aina hii huchukia na kukereka wakiomba Ramadhan imalizike haraka ili warudi katika maovu.

Bila shaka hawa ni miongoni mwa waliopata hasara kwa kuwa funga zao zimekosa unyenyekevu na Ikhlas (matarajio ya kulipwa thawabu na Allah). Allah Mtukufu anasema: "Na wala hawakuamrishwa ila wamwabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia Dini." [Qur'an, 98:5].

Aya hii inaonesha uhusiano uliopo baina ya matendo (amali) ya mja na Ikhlas. Kama zilivyo ibada nyingine, pia swaumu ya Ramadhan ina nguzo, masharti na sunna zake. Ibada ya swaumu hupata maana yake halisi pale mfungaji anapolinda funga yake kwa kujiepusha na mambo maovu na yenye kupumbaza.

Sambamba na hayo, mfungaji anapaswa kuwa na Ikhlas, kwani Allah hakubali amali ya mtu ila ile ambayo imekusudiwa kwake kwa nia, Ikhlas, moyo msafi, pamoja na kuzingatia mwenendo wa Mtume wake Muhammad (rehema na amani iwe juu yake).

Ikhlas itakapoondoka, funga ya mja hugeuka kuwa amali isiyokuwa na malipo yoyote kwa Allah. Na si hivyo tu, mfungaji atakemewa, kukaripiwa, kufedheheshwa na kuadhibiwa siku ya Kiyama.

Kudumisha ibada baada ya Ramadhan

Kwa upande mwingine, ni muhimu kujiuliza kama unaendeleza ibada ulizokuwa ukifanya wakati wa Ramadhan. Ikiwa umerejea kwa kasi katika maasi au kuzembea katika ibada, hiyo ni ishara kwamba mafunzo ya Ramadhan hayajapenya vilivyo ndani ya moyo wako.

Kama ambavyo ulijipinda kufanya ibada mbalimbali katika mwezi wa Ramadhan, unapaswa kuweka malengo madogo lakini endelevu, kama kusoma Qur'an kila siku na kutekeleza ibada ya sala kwa nidhamu ile ile uliyoionesha ndani ya Ramadhan.

Kwa upande wa maadili, Ramadhan imetufunza uaminifu, unyenyekevu na kuepuka vitendo vibaya, kama vile kusema uongo, kusengenya, kuzini, kunywa pombe, kutafuta fedha kwa njia za haramu, na kadhalika.

Baada ya Ramadhan tunapaswa kuangalia kama tabia hizi mbaya tumeziacha. Hii ni kwa sababu, maadili ya dini yanapaswa kuwepo katika maisha yetu ya kila siku, na si katika mwezi wa Ramadhan pekee.

Vilevile, tunatakiwa kudumisha ukarimu tuliyouonesha ndani ya Ramadhan, ikiwa ni pamoja na kutoa sadaka na kuwasaidia masikini na wenye uhitaji. Tuendeleze moyo huu wa kuwajali wengine katika miezi mingine.

Pia, tusisahau kufanya tathmini ya bajeti. Katika mwezi wa Ramadhan, baadhi ya watu hutumia fedha nyingi kununua vyakula mbalimbali ambavyo havina ulazima na hatimaye kuishia kuvitupa.

Katika Ramadhan zijazo, 'Insha Allah', ni vyema Muislamu ukafanya tathmini ya bajeti ya futari na mahitaji mengine, isiyokuwa na ufujaji (israf), na kuepuka matumizi yasiyo ya lazima, kwani "Hakika yeye (Mwenyezi Mungu) hawapendi wanaofanya israf." [Qur'an, 7:31].

شوّال

MAKALA MAALUM
SHEIKH Seif Ruga
0712 690 811

Mafunzo muhimu ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan

Mwezi Mtukufu wa Ramadhan umeondoka, ukiwaacha watu katika hali tofauti, baadhi wakiwa na furaha na wengine wakiwa na huzuni. Mwenye furaha ni yule aliyepata rehema za Allah Mtukufu, msamaha wake na kuepushwa na Moto; na mwenye huzuni ni yule aliyezembea na kukosa msamaha wa madhambi yake. Ingawa Ramadhan imepita, mlango wa mema haujafungwa, kwani fursa za kuchuma kheri zinaendelea kila wakati. Hivyo, ni jukumu la kila Muislamu kutumia vyema kila nukta ya wakati wake katika ibada na kutafuta ridhaa ya Allah.

Aliyekuwa anamuabudu Allah katika mwezi wa Ramadhan tu, basi Ramadhan imetoweka; na aliyekuwa anamwabudu Allah wakati wote, hakika Allah yuko hai milele na hatoweki.

Mwezi wa Ramadhan umetupa funzo la uchamungu na kuwa karibu na Allah. Kwa sababu hiyo, tunatakiwa tuyaishi mema yote tuliyojipamba nayo katika mwezi wa Ramadhan. Sahaba mmoja alimtaka Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie) amfahamishe jambo moja tu ambalo akishikamana nalo katika maisha yake yote, hatohitaji ufafanuzi wa mtu mwingine.

Mtume alimwambia: "Sema, 'Nimemuamini Allah,' kisha kuwa na msimamo imara katika kile unachoamini..." Sasa ndugu yangu Muislamu, jiulize baada ya Ramadhan utaendelea kusoma Qur'an, kutoa sadaka na kusimama usiku kwa dua na ibada? Au utafuata njia ya shetani aliyefungwa pingu katika mwezi wa Ramadhan?

Mtume wa Allah ametutahadharisha juu ya kuacha ibada tulizozoea kufanya. Siku moja alimwambia Abdillah bin Umar: "Ewe Abdillah! Usiwe kama fulani, anasimama usiku kufanya ibada, kisha anaacha." Kadhalika, Mtume amesema: "Hakika amali zinazopendwa zaidi na Allah ni zile za kudumu hata kama ni chache."

Wanazuoni wa Kiislamu wameeleza kuwa, miongoni mwa alama za kukubaliwa ibada za mwezi wa Ramadhan ni kuendelea na ibada baada yake. Kheri hubeba kheri nyingine na amali njema hufuatiwa na nyingine. Mja hujipamba na uchamungu, utulivu, heshima, shukrani na kujikurubisha kwa Allah hata baada ya kumalizika mwezi wa Ramadhan.

Iwapo mja atarejea katika maovu na kuacha ibada, basi hiyo si alama ya kheri wala wema. Wema waliotangulia waliwafananisha watu wanaoacha mema baada ya Ramadhan na wale wasiomjua Allah isipokuwa katika Ramadhan tu.

Allah Ta'ala anatukumbusha na kututahadharisha tusiwe kama yule mwanazuoni wa Bani Israil, Bilam bin Baura, ambaye alipata ladha ya imani na ishara kutoka kwa Allah Mtukufu, kisha akageuka na kuchagua upotofu:

"Na wasomee habari za yule ambaye tulimpa ishara zetu, naye akajivua nazo. Na shetani akamuandama, akawa miongoni mwa waliopotea." [Qur'an, 7:175].

Utekelezaji wa ibada unahitaji juhudi kubwa na uvumilivu. Ni mapambano ya kudumu katika kutekeleza yaliyoamrishwa na kuacha yaliyoharamishwa, ni vita ya mtu dhidi ya nafsi yake na dhidi ya shetani.

Allah anasema: "Na wanaofanya juhudi kwa ajili yetu, Sisi tutawaongoa kwenye njia zetu. Na hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na watu wema." [Qur'an, 29:69]. Imam Ahmad (Allah amrehemu) aliulizwa ni wakati gani mja atapata raha halisi. Akajibu: "Mtu hupata faraja na raha halisi pale tu anapoweka mguu wake Peponi."

Naye Imam Shafi (Allah amrehemu) amesema: "Mtu mwenye heshima hawezi kupata faraja na raha halisi hapa duniani. Maisha haya ni ya juhudi na mapambano hadi mja atakapokutana na Mola wake." "Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie yakini (mauti)." [Qur'an, 15:99].

Mafundisho ya Uislamu yanabainisha kuwa ibada haziishi kwa kumalizika msimu mmoja. Katika Uislamu, kila msimu wa kheri unapotamatika, hufuatiwa na mwingine.

Kumalizika kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhan kunafuatiwa na msimu wa Hijja, ibada inayotekelezwa katika miezi maalumu, kama Allah Ta'ala anavyobainisha: "Hijja ni miezi maalumu..." [Qur'an, 2:197].

Na mwanzo wa ibada ya Hijja ni kuingia kwa mwezi wa Shawwal (Mfungo mosi). Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "Atakayefunga mwezi wa Ramadhan, kisha akafuatisha na funga ya siku sita za mwezi wa Shawwal, ni sawa na mtu aliyefunga milele."

Kufunga siku sita za Shawwal ni fursa adhimu kwa Muislamu kuendelea na ibada baada ya Ramadhan. Ni kitendo cha kuonesha shukrani kwa Allah kwa kukuwezesha kuikamilisha Ramadhan, na pia huongeza thawabu na kurekebisha kasoro zilizojitokeza katika swaumu ya Ramadhan.

Kama sala za sunna zinavyosaidia kufidia upungufu unaojitokeza katika sala za faradhi, vivyo hivyo kufunga siku sita za Shawwal hurekebisha kasoro zilizojitokeza katika swaumu ya Ramadhan.

شوّال

KALAMU HURU

SEHEMU YA 2

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

SUBIRA – somo kuu la Ramadhan

Baada ya Muislamu kujifunza na kujenga uchamungu (taqwa) ndani ya mwezi wa Ramadhan, kuna somo jingine muhimu sana analotoka nalo katika mwezi huu mtukufu. Somo hilo ni subira. Kwa hakika, ibada ya swaumu haiwezekani bila subira. Ndiyo maana wanazuoni wameeleza kwamba swaumu ni nusu ya subira, na subira ni nusu ya imani.

Maana na aina ya subira

Subira ni uwezo wa nafsi kustahimili na kudhibiti hisia zake katika hali mbalimbali za maisha. Ni uwezo wa kujizuia kufanya yale yasiyompendeza Mwenyezi Mungu, kuvumilia katika kufanya mema, na kukubali kwa moyo mkunjufu yale yanayokadiriwa na Allah.

Hata kama jambo linamuumiza mtu au linamletea ugumu, subira humfanya abaki thabiti katika uongofu. Wanazuoni wameigawa subira katika sehemu kuu tatu.

Subira ya kwanza ni subira katika kumtii Mwenyezi Mungu. Hii ni pale mtu anapojilazimisha kufanya ibada kama swala, swaumu, kusoma Qur'an na sadaka hata kama kuna ugumu. Subira ya pili ni subira ya kujiepusha na maasi. Hii ni pale mtu anapojizuia na mambo aliyoyaharamisha Allah licha ya vishawishi vya nafsi na dunia.

Subira ya tatu ni subira juu ya mitihani na makadirio ya Allah. Hii ni pamoja na kuvumilia magonjwa, matatizo ya maisha, au changamoto za kiuchumi.

Ramadhan ni chuo cha subira

Ndani ya mwezi wa Ramadhan, aina zote hizi za subira huonekana kwa uwazi mkubwa. Muislamu anapofunga huvumilia njaa na kiu kwa muda mrefu. Hii ni subira juu ya makadirio ya Allah. Anapodumu katika swala, kusoma Qur'an na kufanya ibada nyingine, hii ni subira katika utiifu. Na anapojiepusha na matamanio na maasi, hii ni subira dhidi ya maovu.

Kwa maana hiyo, Ramadhan ni chuo kikuu cha mafunzo ya subira kinachomjenga Muislamu kuwa imara kiroho na kimaadili.

Changamoto baada ya Ramadhan

Changamoto kubwa huanza baada ya Ramadhan kuondoka. Swali muhimu ni hili: je, subira tuliyojifunza inaendelea au inaishia pamoja na mwezi wa Ramadhan?

Katika maisha ya kila siku, mwanadamu hukutana na changamoto nyingi. Kuna matatizo ya kifamilia, shinikizo la kazi, mitihani ya kiuchumi na vishawishi vya kila aina. Bila subira, ni rahisi sana mtu kukata tamaa au kufanya maamuzi mabaya.

Subira katika mawasiliano na ibada

Moja ya maeneo muhimu yanayohitaji subira ni mawasiliano na watu. Migogoro mingi hutokea si kwa sababu ya matatizo makubwa, bali kwa sababu ya kukosa subira katika maneno na vitendo.

Muislamu anatakiwa ajifunze kunyamaza pale inapobidi, kusamehe na kuvumilia makosa ya wengine. Haya yote ni sehemu ya tabia njema ambazo Uislamu unazihimiza.

Kwa upande mwingine, baada ya Ramadhan, hamasa ya ibada mara nyingi hupungua. Hata hivyo, hapa ndipo subira inahitajika zaidi. Muislamu anatakiwa ajilazimishe kuendelea kuswali kwa wakati, kusoma Qur'an na kufanya ibada nyingine hata kama hana ile ari aliyokuwa nayo ndani ya Ramadhan.

Subira, nguvu ya ndani

Ni muhimu kufahamu kwamba subira si udhaifu. Kinyume chake, subira ni nguvu kubwa ya ndani.



Mtu mwenye subira ana uwezo wa kuhimili mambo ambayo wengine hushindwa. Ana utulivu wa moyo na anaishi kwa matumaini akijua kwamba kila jambo lina hikma yake. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu Amewaahidi malipo makubwa wale wenye subira.

Baada ya Ramadhan, kila Muislamu anapaswa kujiuliza: Je, subira yangu imeongezeka?

Je, nina uwezo mkubwa zaidi wa kudhibiti nafsi yangu?

Ikiwa jibu ni ndiyo, basi hiyo ni dalili njema kwamba swaumu yake imeleta mabadiliko chanya katika maisha yake.

Lakini safari ya malezi ya nafsi haishii hapa. Mbali na uchamungu na subira, kuna silaha nyingine muhimu ambayo Muislamu hujenga ndani ya Ramadhan nayo ni udhibiti wa nafsi.

Katika makala inayofuata, tutachambua kwa kina somo hili muhimu la kujidhibiti na jinsi linavyoweza kumsaidia Muislamu kuishi maisha ya nidhamu na mafanikio baada ya Ramadhan.

شوّال

TUJIFUNZE

AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama

Namna AI inavyotumika katika uandishi wa habari

Katika enzi hii ya teknolojia, uandishi wa habari umepata mageuzi makubwa kutokana na kuingia kwa akili bandia (Artificial Intelligence – AI). Kwa muda mrefu, waandishi wa habari walitegemea sana uwezo wao wa kibinafsi kukusanya taarifa, kuchambua data na kuandika habari kwa mkono.

Lakini leo, mambo yamebadilika kwa kiasi kikubwa. AI imeleta kasi, ufanisi na uwezo mkubwa wa kuchakata taarifa nyingi kwa muda mfupi, na hivyo kuwawezesha waandishi kufanya kazi zao kwa urahisi zaidi.

Hata hivyo, licha ya mabadiliko haya ya kiteknolojia, jukumu la mwisho la kuhakikisha ukweli, usahihi na maadili katika habari bado liko mikononi mwa mwanadamu—mhariri na mwandishi mwenyewe.

Ufuatiliaji wa habari kwenye fani mahususi

Kila mwandishi wa habari huwa na eneo lake maalum la ufuatiliaji, linalojulikana kama 'beat'. Hili linaweza kuwa ni siasa, uchumi, michezo, afya au teknolojia. Changamoto kubwa kwa mwandishi ni kufuatilia idadi kubwa ya habari zinazojitokeza kila siku katika eneo lake.

AI imekuja na suluhisho la kipekee kwa tatizo hili kupitia mifumo ya kukusanya na kufupisha habari. Zana kama ChatGPT, Perplexity na nyingine zinaweza kutafuta habari mpya kuhusu mada fulani, kuzichuja na kutoa muhtasari mzuri unaomsaidia mwandishi kuelewa kwa haraka kinachoendelea.

Badala ya kutumia saa nne au tano kusoma makala nyingi, mwandishi anaweza kupata muhtasari mfupi unaomwonyesha habari muhimu zaidi kwa kazi yake. Zaidi ya hayo, teknolojia hii inaweza kubinafsisha taarifa kulingana na mada anazozifuatilia mwandishi.

Uandishi unaotegemea data na uchimbaji wa taarifa

AI imeleta mageuzi makubwa katika uandishi wa habari unaotegemea data na uchambuzi wa kina. Kupitia mbinu inayojulikana kama 'data mining', ambayo hutumia algorithimu za kujifunza kwa mashine, vyombo vya habari vinaweza sasa kuchambua seti kubwa za data na kubaini mifumo au mienendo ambayo si rahisi kuiona kwa macho ya kawaida.

Hii ni muhimu sana katika uandishi wa habari za uchunguzi na uandishi unaotegemea takwimu. Kwa mfano, AI inaweza kuchambua maelfu ya nyaraka za serikali, rekodi za kifedha, au data za uchaguzi ili kubaini mwenendo unaoweza kuwa habari muhimu kwa umma.

Pamoja na hayo, AI hutumika katika uchanganuzi wa kutabiri (predictive analytics), unaotumia data za zamani kujaribu kutabiri matukio ya baadaye. Ingawa hakuna utabiri usio na makosa, hii inawasaidia waandishi kuelewa mwenendo mbalimbali wa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Urahisi wa kufupisha na kusambaza habari

AI pia imebadilisha namna habari zinavyofupishwa na kusambazwa. Vyombo kadhaa vya habari duniani tayari vinatumia AI kuunda muhtasari wa habari ndefu, ili kuwasaidia wasomaji kupata taarifa muhimu kwa haraka.

Mfano mzuri ni huduma ya Minutes by Nikkei, inayotumia mfumo wa AI uitwao Nikkei Tailor kufupisha habari muhimu za biashara na kuzitoa kwa wasomaji kwa muundo mfupi unaofaa kusomwa kwenye simu.

Mfumo huu umepunguza kwa karibu nusu muda ambao waandishi hutumia kuandaa rasimu za habari. Magazeti mengine pia yameanza kutumia mifumo inayowapa wasomaji uhuru wa kuchagua namna wanavyotaka kusoma habari—iwe kwa muhtasari mfupi, kwa maswali na majibu, au kwa maelezo ya kina.

Teknolojia ya sauti, tafsiri na ushirikiano

AI imeongeza uwezo wa vyombo vya habari kufikia hadhira pana kwa kutumia teknolojia ya sauti na tafsiri.

Teknolojia ya 'text-to-speech' inaweza kubadilisha maandishi ya habari kuwa sauti inayofanana na ile ya binadamu, jambo linalowasaidia wasomaji wenye changamoto za kusoma au wale wanaopendelea kusikiliza. Pia, tafsiri za AI zimewezesha vyombo vya habari kufikisha habari kwa lugha nyingi kwa harasa, kama vile gazeti la Le Monde linalotumia teknolojia hii kuchapisha habari kwa lugha mbalimbali.

شَوَّال

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 1

SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)

VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

Hakuna simulizi iliyotajwa mara nyingi zaidi katika Qur'an kama simulizi za Wana wa Israil, Mtume Musa (amani ya Allah imshukie) na mtawala jabari wa zama hizo, Fir-aun. Vilevile, Musa ndiye Mtume pekee ambaye historia yake imetajwa kuanzia kuzaliwa kwake katika Qur'an.

Habari za Mitume wengine mara nyingi huanza pale walipokuwa tayari wametumwa kwa watu wao. Aidha, jina "Musa" ndilo jina lililotajwa mara nyingi zaidi katika Qur'an. Inasemekana limetajwa takribani mara 136 katika sura 34, wakati jina "Ibrahim" limetajwa mara 69, "Nuhu" mara 43, "Isa" mara 25, na "Muhammad" mara nne.

Mtume Musa (amani ya Allah imshukie), Msemezwa wa Allah, ni katika Mitume Watano Wakuu wanaojulikana kama Ulul-'Azmi.

Katika makala hii tutaanza simulizi ya Mtume huyu mtukufu kwa kufuata mpangilio unaopatikana katika Qur'an. Tutatazama hali ya Wana wa Israil baada ya kuondoka kwa Mtume Ya'qub (amani ya Allah imshukie) na mwanawe Yusuf (amani ya Allah imshukie), kabla ya kuanza kwa historia ya Mtume Musa.

Hali ya Wana wa Israil baada ya kuondoka Ya'qub na Yusuf

Qur'an inaeleza kuwa baada ya Mtume Yusuf (amani ya Allah imshukie) kuchaguliwa kuwa msimamizi mkuu wa hazina katika nchi ya Misri, aliileta familia yake kutoka Kan'an kuja kuishi Misri.

Aliwaambia ndugu zake waliokuja kwake kutafuta chakula: "Nendeni na kanzu yangu hii na muiweke mbele ya uso wa baba yangu, naye atapata kuona; na nijieni na watu wenu wote pamoja."

[Qur'an, 12:93]

Qur'an inaeleza pia: "Basi walipoingia kwa Yusuf aliwakumbatia wazazi wake na akasema: "Ingieni Misri, inshaAllah mtakuwa katika amani." [Qur'an, 12:99]. Wana wa Israil waliishi Misri maisha ya amani, heshima na utulivu kwa kipindi kirefu. Baadaye Mtume Ya'qub akafariki dunia, na muda si mrefu mwanawe Yusuf naye akafariki.

Baada ya muda kupita, hali ya Wana wa Israil ilianza kubadilika. Wengi wao walitelekeza misingi ya dini na kuingia katika maisha ya anasa na dhuluma. Watu wa Misri nao wakaanza kuwatazama kwa jicho la dharau. Hatimaye walibaki wakijinasibisha tu na wazazi wao watukufu.

Zaidi ya hayo, Wamisri waliwaona kama wageni waliokuja kutoka nchi nyingine na wakaona hawakuwa na haki ya kuongoza au kutukuzwa katika nchi hiyo.

Utawala wa Mafirauni nchini Misri

Katika kipindi hicho, utawala wa Misri uliingia chini ya wafalme waliokuwa wakijulikana kama Mafirauni (Pharaohs). Mfalme mmoja alifuatia mwingine katika kiti cha ufalme.

Wafalme hao wa Kiqibtwi waliwachukia sana Wana wa Israil. Baada ya kupita kwa muda mrefu, Misri ikatawaliwa na mtawala wa mwisho katika mlolongo huo wa watawala. Huyu ndiye ambaye Qur'an imemtaja kwa jina la Firauni, aliyekutana na Mtume Musa (amani ya Allah imshukie).

Dharau, kiburi na ukatili wa mfalme huyu dhidi ya Wana wa Israil vilizidi sana. Aliwabagua na kuwaweka katika daraja la chini. Wengi wao waliwekwa magerezani, wengine wakateswa na kuuawa. Qur'an inaeleza: "Hakika Fir-aun alitakabari katika ardhi na akawafanya watu wake makundi mbalimbali."

[Qur'an, 28:4].

Fir-aun kuwachinja watoto wa kiume

Katika kipindi hicho, mmoja wa makuhani wa Firauni alimpa habari kwamba hivi karibuni angezaliwa mtoto wa kiume miongoni mwa Wana wa Israil ambaye angeuangusha utawala wake. Firauni alishtushwa sana na habari hiyo.

Kwa kuwa alimwamini sana kuhani huyo, alichukua hatua kali ili kuzuia tukio hilo lisitokee. Aliamuru kwamba watoto wote wa kiume watakaozaliwa katika familia za Wana wa Israil wauwawe mara tu wanapozaliwa.

Qur'an inaeleza: "...akiwachinja watoto wao wa kiume na kuwaacha hai wanawake wao. Hakika yeye alikuwa miongoni mwa waharibifu wakubwa." [Qur'an, 28:4]. Askari walipewa jukumu la kufuatilia wanawake wajawazito katika jamii ya Wana wa Israil. Kila mtoto wa kiume aliyekuwa akizaliwa aliuawa.

Agizo hili lilisababisha maelfu ya watoto wasio na hatia kuchinjwa, jambo lililoleta huzuni kubwa na vilio kwa mama zao. Kwa siku, makumi ya watoto walikuwa wakichinjwa kama wanavyosinjiwa kondoo siku ya Idi.

Katika Qur'an, Allah anawakumbusha Wana wa Israil kwa kusema: "Na kumbukeni tulipowaokoa kutoka kwa watu wa Firauni waliokuwa wakikupeni mateso mabaya, wakiwachinja watoto wenu wa kiume na kuwaacha hai wanawake wenu. Na katika hayo kulikuwa na mtihani mkubwa kutoka kwa Mola wenu."

[Qur'an, 2:49].

Kuzaliwa kwa Mtume Musa (Amani ya Allah imshukie)

Allah anapotaka jambo, hulifanyia sababu. Alitaka kuwatoa Wana wa Israil kutoka katika minyororo ya utumwa na mateso na kuwarejeshea heshima yao.

Alitaka pia kuuangusha utawala wa Mafirauni uliodumu kwa zaidi ya miaka elfu tatu tangu kuunganishwa kwa miji mbalimbali ya

شوال

MAKALA YA AFYA
0764 101 018

SEHEMU YA 2

DKT.
Omar A. Kasuwi
Daktari Bingwa Mshauri wa magonjwa Moyo!
Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA)

Kupanda BP nyakati za usiku, hatari nyingine kubwa iliyofichika!

Katika sehemu ya kwanza ya makala hii, tuliona kuwa watu wengi hupima shinikizo la damu mchana au wanapojisikia vibaya, lakini utafiti wa 2024–2025 unaonyesha kwamba kupima usiku, ni muhimu zaidi kuliko nyakati za mchana. Tulijifunza pia kuhusu miundo isiyo ya kawaida ya mabadiliko ya BP usiku ambayo ina tafsiri kadhaa kutegemea na aina ya mabadiliko yenyewe huku pia tukichungulia takwimu kuona zinasemaje? Leo tunamaliza makala kwa kuona hatari za shinikizo la damu (BP) nyakati za usiku .

Visababishi vya shinikizo la damu nyakati usiku

Kisababishi kikuu ni mtindo wa maisham ukihusisha msongo wa mawazo endelevu, unywaji wa vilevi nyakati za usiku, tabia ya kula chakula kupita kiasi muda mfupi kabla ya kulala, matumizi ya vinywaji vyenye kaffein, na matumizi ya chumvi nyingi.

Visababishi vingine ni pamoja na magonjwa kama kisukari, figo, kukosa usingizi kwa muda mrefu, shida ya kupumua nyakati za usiku, magonjwa ya moyo, na watu wenye umri wa miaka zaidi ya 65 ambao mara nyingi wanapata tatizo la kushindwa kulala.

Je utajuaje kama una BP ya usiku?

Njia pekee itakayokuwezesha kutambua hali ya shinikizo lako la damu nyakati za usiku ni kujenga tabia ya kujipima shinikizo la damu (BP) kabala hujalala kwa kutumia mashine ya kupimia shinikizo la damu (BP) kila siku nyumbani.

Njia nyingine ni kufungwa kifaa/kipimo kitakacho rekodi shinikizo la damu (BP) kwa masaa 24 (ABPM). Pia, unaweza kufungwa kifaa kitakachorekodi shinikizo la damu nyakati za usiku pekee (night-time BP devices).

Dalili za kupanda shinikizo la damu usiku

Dalili za kukosa usingizi (Insomnia) ni pamoja na kushindwa kuanza au kudumisha usingizi; usingizi usiotulia yaani kuamka mara kwa mara usiku, kugeuka-geuka kitandani na ndoto mbaya au nzito zinazoweza kuvuruga usingizi wako.

Dalili nyingine ni kuamka bila kujisikia umepona hata baada ya kulala muda wa kutosha, kuamka ukiwa na maumivu ya kichwa yanayopungua kadiri siku inavyoendelea na kujisikia mchovu kupita kiasi nyakati za mchana.

Dalili nyingine ni kusinzia mara kwa mara, hata baada ya kulala usiku; kupungua kwa umakini, kumbukumbu na uwezo wa kufanya kazi; wasiwasi au msisimko wa ghafla nyakati za usiku; kutokwa na jasho jingi wakati wa usingizi na kuhisi joto kali au "hot flashes" bila sababu ya wazi.

Hatari za shinikizo la damu (BP) nyakati za usiku

Mosi, kupatwa na kiharusi

Hii inatokana na BP kupanda nyakati za usiku badala ya kushuka (reverse dippers) jambo ambalo uhatari wake ni mara tatu zaidi ya kiharusi kinachotokana na ubongo kukosa hewa ya kutosha ya Oksijeni na damu kuganda kwenye mishipa ya artery (ischemic stroke.)

Kiharusi pia kinaweza kutokana na shinikizo la damu (BP) kutoshuka na kubaki juu kwa asilimia 10 hadi 20 (non-dippers) hali ambayo uhatari wake ni mara mbili zaidi ya kiharusi kinachotokana na ubongo kukosa hewa ya kutosha ya oksijeni sehemu ya ubongo (lacunar stroke.)

Kiharusi pia kinaweza kutokana na shinikizo la damu (BP) kushuka zaidi ya asilimia 20 kwa nyakati za usiku ukilinganisha na mchana (extreme dippers) hali ambayo ni hatari zaidi ya kiharusi kinachotokana damu kuganda kwenye ubongo "ischemia".

Hali ya kushuka BP zaidi ya asilimia 20 kwa nyakati za usiku inasababisha uharibifu wa mishipa midogo, kupungua kwa uwezo wa ubongo kudhibiti mtiririko wa damu na kuongezeka kwa shinikizo nyakati za mapema asubuhi.

Pili, kudhoofika ama kushindwa kwa moyo kufanya kazi

Hali hii inatokana na kuongezeka kwa mzigo wa damu nyakati za usiku na moyo kulazimika kutumia nguvu ya ziada. (afterload).

Kwa sababu hiyo, ipo hatari ya kulazwa hospitalini kwa sababu ya kushindwa kwa moyo (heart failure) huongezeka kwa asilimia 40 hadi 60 na kuzidi migongano ya moyo na figo (cardiorenal syndrome).

Tatu, mshituko ama shambulio la moyo (myocardial infarction)

Shinikizo la damu (BP) linapokuwa juu nyakati za usiku (>130 mmHg) huongeza hatari ya kupata shambulio la moyo muda huo. Hali hiyo pia inaongeza uwezekano wa damu kuganda nyakati za asubuhi (Thrombosis).

Kwa mujibu wa taarifa ya American Heart Association 2024, SBP nyakati za usiku ni kiashiria madhubuti zaidi cha hatari ya moyo!

شوّال

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

Ubora na faida za kudumu katika ibada

Kutoka kwa mama Aisha (Allah amuwie radhi) amesimuliwa kuwa, siku moja Mtume (rehema na amani zimshukie) alimwambia: "Ewe Aisha, je mna chakula chochote?" Akamjibu: "Ewe mjumbe wa Allah, hatuna chochote." Mtume akasema: "Basi mimi ninafunga."

Mama Aisha anaeleza kuwa, baadaye Mtume (rehema na amani zimshukie) aliondoka, kisha wakaletewa zawadi. Mtume aliporejea akamwambia: "Ewe mjumbe wa Allah! Tumeletewa zawadi, na nimekuhifadhia kitu."

Mtume akauliza: "Kitu gani hicho?" Mama Aisha akamjibu: "Ni hais (chakula kilichotengenezwa kwa tende, maziwa yaliyokaushwa (aqt) na samli)." Mtume akasema: "Niletee." Akaletewa chakula hicho, akala, kisha akasema: "Niliamka asubuhi nikiwa nimefunga."

Talha (Allah amridhie) amesema alimweleza Mujahid kuhusu hadith hii, naye akasema: "Hii ni kama mtu anayetoa sadaka katika mali yake; akitaka anaendelea nayo (anatoa sadaka), na akitaka anaacha." [Imenukuliwa na Muslim].

Mafundisho ya hadith

Hadith hii inatufundisha kuwa kudumisha ibada ni miongoni mwa sifa za waumini wa kweli. Ni hivi karibuni tu tumetimiza swaumu ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan kwa taufiki ya Allah Ta'ala.

Kumalizika kwa Ramadhan hakuashirii mwisho wa ibada ya funga kwa mwaka huu, la hasha. Ibada ya funga ipo wakati wote na siku zote. Imethibiti kuwa Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa akinuia kufunga asubuhi baada ya kuamka, pale alipokuta hakuna chakula nyumbani kwake.

Kwa hiyo, tusingoje hadi Ramadhan nyingine iingie ndipo tufunge. Kwa kuacha kufunga sunna, tunajikosesha thawabu nyingi zinazopatikana ndani yake.

Miongoni mwa mambo muhimu katika maisha ya Muislamu ni kuendeleza utiifu na ibada katika nyakati zote ili hatimaye apate mwisho mwema (ḥusnul khātima).

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Allah anapomtakia kheri mja wake humtumia kabla ya kufa kwake." Masahaba wakauliza: "Ewe Mtume wa Allah, vipi humtumia?" Akasema: "Humuwezesha kufanya amali njema kisha humfisha akiwa juu ya amali hiyo." [Tirmidhi].

Hivyo basi, yatupasa kutekeleza ibada wakati wote na katika hali zote – iwe wakati wa furaha au dhiki, ndani ya Ramadhan na nje ya Ramadhan, wakati wa neema au shida, na katika mitihani au raha. Kufanya ibada wakati wa fitina na machafuko kuna malipo makubwa mbele ya Allah, kama alivyosema Mtume: "Ibada wakati wa fitina na machafuko ni kama kuhamia kwangu." [Tirmidhi].

Hii ina maana kuwa ibada anayofanya mtu wakati wa fitina na kuchanganyika kwa mambo ina ujira sawa na ule waliopata Masahaba waliohama kutoka Makka kwenda Madina katika zama za Mtume (rehema na amani zimshukie).

Anayedumu katika ibada wakati mazingira hayamhamasishi kufanya hivyo, au wakati watu wengi wamerudi katika uvivu na uzembe baada ya Ramadhan, bila shaka atapata ujira mkubwa mbele ya Allah.

Tuthibitishe malengo ya funga

Ibada yoyote ambayo Allah Mtukufu ameifaradhisha ina malengo makuu ambayo tunapaswa kuyafikia. Ibada ya funga imewajibishwa ili tufikie kilele cha uchamungu. Tusipozishughulisha nafsi zetu na uchamungu, tutakuwa tunatangaza wazi kuwa ibada ya funga haikuwa na taathira yoyote katika nafsi zetu.

Mtume (rehema na amani zimshukie) ametuusia kushikamana na uchamungu katika hali zote na mazingira yote, na ametuelekeza yale yanayotufaa katika uhusiano wetu na Mwenyezi Mungu, pamoja na uhusiano wetu na watu wengine.

Kutoka kwa Abu Dharr (radhi za Allah ziwe juu yake) amesema, mjumbe wa Allah (rehema na amani zimshukie) alimwambia: "Mche Allah popote ulipo, na fuatisha ubaya kwa wema utafuta (huo ubaya), na ishi na watu kwa tabia njema." [Tirmidhi].

Hadith nyingine iliyosimuliwa na Abu Huraira (radhi za Allah ziwe juu yake) inaeleza kuwa, siku moja Mtume (rehema na amani zimshukie) aliulizwa: "Ni jambo gani litakalowaingiza watu wengi zaidi Peponi?" Akasema: "Ni kumcha Mungu (taqwa) na kuwa na tabia njema." [Ahmad, na imesahihishwa na Ibn Hibban].

Uchamungu hutuweka katika mazingira bora ya kuimarisha mafungamano yetu na Allah, na tabia njema ndiyo kiunganishi imara baina ya watu.

JUNAYNAT ALLY DAMA

Somo la malezi kutoka uzoefu wa wakinamama duniani

Malezi ya watoto ni jukumu linalofanana karibu katika kila jamii duniani. Ingawa tamaduni hutofautiana, wazazi wengi wanakutana na changamoto zinazofanana: kuwalea watoto wenye maadili, kuwajenga kisaikolojia na kuwasaidia kuwa watu wanaojitegemea.

Katika makala iliyoandikwa na Zakeeya Ali, yenye kichwa "Parenting Tips from Moms Around the World," akina mama kutoka sehemu mbalimbali duniani walishiriki uzoefu na mbinu zao za malezi. Ushauri wao unaonyesha kwamba, licha ya tofauti za kitamaduni, kuna kanuni kadhaa za msingi zinazoweza kuwasaidia wazazi wengi katika safari ya malezi.

Watoto hujifunza kupitia mfano wa wazazi

Moja ya mafunzo muhimu katika makala hiyo ni kwamba watoto hujifunza zaidi kwa kuangalia matendo ya wazazi wao kuliko kusikiliza maelekezo yao. Hii ina maana kwamba maadili kama uaminifu, heshima na huruma hujengwa zaidi kupitia tabia za wazazi. Wazazi wanapowaonyesha watoto wao jinsi ya kuzungumza kwa heshima, kuwajali wengine na kuwajibika, watoto huiga tabia hizo kwa urahisi.

Tumia muda wa ubora na watoto

Akina mama wengi walisisitiza umuhimu wa kutumia muda na watoto. Hapa si lazima iwe muda mwingi sana, bali ni muda wenye ubora. Shughuli rahisi kama kusoma hadithi pamoja, kucheza au kuzungumza kuhusu siku ya mtoto zinaweza kuimarisha uhusiano wa familia na kumfanya mtoto ajisikie kuthaminiwa.

Nidhamu yenye upole na maelezo

Katika ushauri uliotolewa, wazazi wanahimizwa kutumia nidhamu yenye maelezo badala ya ukali. Mtoto anapokosea, ni muhimu kumweleza kwa nini kitendo hicho si sahihi badala ya kumwadhibu bila maelezo. Mbinu hii humsaidia mtoto kuelewa matokeo ya matendo yake na kujifunza kufanya maamuzi bora.

Fundisha watoto kuwajibika

Ushauri mwingine ni kuwafundisha watoto kuwajibika mapema. Hii inaweza kufanywa kwa kuwapa majukumu madogo ya nyumbani kulingana na umri wao. Watoto wanaposhiriki katika kazi za familia, hujifunza thamani ya uwajibikaji, ushirikiano na kujitegemea.

Sikiliza watoto wako

Akina mama wengi pia wanashauri wazazi kujenga utamaduni wa kusikiliza watoto. Watoto wanapopata nafasi ya kueleza mawazo na hisia zao bila kuogopa kukataliwa, wanajifunza kujiamini na kuwa wazi katika mawasiliano. Mazungumzo haya pia huwasaidia wazazi kuelewa mahitaji ya kihisia ya watoto wao.

Heshimu utu wa mtoto

Katika malezi bora, mtoto anapaswa kutazamwa kama mtu mwenye hisia na mawazo yake. Kuwaheshimu watoto kwa kuzingatia maoni yao au kuwapa nafasi ya kuchagua katika mambo madogo ya maisha huwasaidia kukuza uwezo wa kufanya maamuzi na kujithamini.

Kukuza uhuru wa mtoto

Ushauri mwingine unaojitokeza ni kuwapa watoto nafasi ya kujifunza kufanya mambo wenyewe. Wazazi wanapowaruhusu watoto kujaribu, kufanya makosa na kujifunza kutokana na makosa hayo, wanasaidia kujenga ujasiri na uwezo wa kujitegemea.

Weka mipaka iliyo wazi

Ingawa upendo na uhuru ni muhimu, wazazi pia wanahimizwa kuweka mipaka ya wazi. Watoto wanahitaji kuelewa ni tabia zipi zinakubalika na zipi hazikubaliki. Mipaka hii inapowekwa kwa utulivu na uthabiti, huwasaidia watoto kujifunza nidhamu na kujidhibiti.

Jenga mazingira ya upendo nyumbani

Ushauri mwingine uliotolewa katika makala hiyo ni umuhimu wa kujenga mazingira ya familia yenye upendo. Watoto wanaokulia katika nyumba yenye mawasiliano mazuri na upendo wa wazazi huwa na afya bora ya kihisia na ujasiri wa kukabiliana na changamoto za maisha.

Subira katika malezi

Hatimaye, akina mama wengi wanasisiti-

MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS

Kwa nini wanaume wengi hukimbia tiba ya kisaikolojia?

Katika miaka ya karibuni, mjadala kuhusu afya ya akili umeongezeka sana duniani. Kampeni nyingi zimehamasisha watu kutafuta msaada wa kitaalamu wanapokabiliwa na changamoto za kihisia au kisaikolojia.

Hata hivyo, tafiti nyingi zinaonyesha kuwa wanaume wako nyuma katika kutafuta tiba ya kisaikolojia ikilinganishwa na wanawake. Swali ni: kwa nini wanaume wengi hukwepa au kuchelewa kuingia katika tiba ya kisaikolojia?

Wataalamu wa saikolojia wanaeleza kwamba sababu si kwamba wanaume hawana matatizo ya kisaikolojia. Badala yake, mara nyingi wanazuiwa na mifumo ya kijamii na kisaikolojia ambayo imejenga mtazamo fulani kuhusu maana ya kuwa mwanaume.

Malezi ya kijamii kuhusu uanaume

Katika jamii nyingi, wavulana hulelewa wakifundishwa kuwa mwanaume lazima awe mwenye nguvu, mwenye kujitegemea na asiyeonyesha udhaifu. Kuonyesha hisia kama huzuni, hofu au kuchanganyikiwa mara nyingi huonekana kama ishara ya udhaifu.

Matokeo yake, wanaume wengi hukua wakiamini kwamba wanapaswa kutatua matatizo peke yao. Kuomba msaada—katika masuala ya kihisia—huonekana kama kushindwa au kupoteza hadhi. Kwa msingi huo, wazo la kwenda kwa mtaalamu wa saikolojia linaweza kuhisiwa kama kuvunja kanuni za uanaume walizofundishwa tangu utoto.

Hofu ya kupoteza uhuru

Sababu nyingine muhimu ni suala la uhuru wa mtu binafsi. Wanaume wengi wamejengewa utamaduni wa kujitegemea na kuwa na udhibiti wa maisha yao. Katika mazingira haya, kwao, kuomba msaada ni kupoteza uwezo wa kudhibiti mambo.

Kwa wanaume wengi, tiba ya kisaikolojia ni hali ambayo mtu mwingine anachukua nafasi ya kuelekeza maisha yao ikiwa ni ishara ya kutokuwa na uwezo wa kushughulikia matatizo yao wenyewe. Kwa sababu hiyo, hujaribu kuvumilia matatizo yao kimya kimya.

Kulinda heshima na hadhi

Kipengele kingine kinachochangia wanaume kukwepa tiba ni kulinda hadhi yao. Wanaume wengi hujiona kama watu wanaopaswa kuwa nguzo katika familia au jamii. Wanaona kukiri kuwa na matatizo ya kisaikolojia ni kupoteza hadhi hiyo.

Kwa mfano, mwanaume ambaye amezoea kuwa mtu anayesaidia wengine anaweza kuona ni vigumu sana kuwa katika nafasi ya kuomba msaada. Katika hali hiyo, anaona tiba ya kisaikolojia ni ishara ya kushindwa badala ya hatua ya kujisaidia.

Mtazamo kuhusu uwezo na mafanikio

Kwa baadhi ya wanaume, utambulisho wao umejengwa juu ya uwezo wa kutatua matatizo. Wamezoea kufikiri kwamba kila changamoto ina suluhisho linalopatikana kupitia juhudi na uvumilivu.

Lakini tiba ya kisaikolojia mara nyingi huanza pale ambapo mtu anakubali kwamba kuna jambo ambalo haliendi vizuri katika maisha yake. Kukubali hali hiyo kunaweza kuwa vigumu kwa wanaume ambao wamejifunza kwamba mwanaume "anapaswa kuwa na majibu kwa kila tatizo."

Kwa sababu hiyo, baadhi yao hujaribu kukimbia hisia zao kwa kujishughulisha kupita kiasi na kazi, matumizi ya pombe, au hasira.

Hofu ya kufungua hisia

Wanaume wengi hawajazoea mazingira ya kuzungumzia hisia zao kwa uwazi. Katika jamii nyingi, wavulana hawahimizwi kuzungumza kuhusu maumivu ya kihisia. Badala yake huambiwa "vumilia" au "kuwa mwanaume."

Kwa sababu hiyo, wazo la kukaa na mtaalamu na kuzungumzia hisia za ndani linaweza kuwa gumu sana. Wengine huogopa kwamba kufungua hisia zao kunaweza kuleta aibu, kukataliwa au kupoteza heshima katika jamii.

Nini kinaweza kusaidia wanaume kukubali tiba

Wataalamu wa saikolojia wanaeleza kuwa ipo haja ya kubadilisha namna tiba hiyo inavyowasilishwa ili kuwasaidia wanaume kukubali kutibiwa. Badala ya kuonekana kama ishara ya udhaifu, tiba inaweza kuwasilishwa kama njia ya kuongeza uwezo wa mtu kushughulikia maisha.

Ni muhimu pia kuhakikisha kwamba mazingira ya tiba yanaheshimu uhuru na hadhi ya mtu. Mchakato wa tiba unapokuwa wa ushirikiano—ambapo mgonjwa anashiriki katika kufanya maamuzi—wanaume wengi hujihisi salama zaidi kuzungumza.

Vilevile, kuwepo kwa vikundi vya wanaume au mifano ya wanaume wanaozungumzia wazi afya ya akili kunaweza kusaidia kupunguza

NA UKHTI FATIMA

Uwekezaji halal: Namna ya kukuza mali kwa kufuata misingi ya Uislamu

Uwekezaji halali ni shughuli ya kuwekeza fedha kwa kufuata sheria na misingi ya Sharia. Kwa lugha rahisi, ni uwekezaji unaohakikisha kwamba njia ya kupata faida haivunji mafundisho ya Uislamu. Hii ina maana kuwa chanzo cha mapato, namna ya kuwekeza, na matokeo ya uwekezaji lazima yawe safi na halali.

Katika mfumo huu, lengo si kupata faida tu bali pia kuhakikisha kuwa faida hiyo inapatikana kwa njia inayokubalika kidini. Uwekezaji halali unakataza mambo kama riba, kamari, na mikataba yenye utata. Aidha, Muislamu haruhusiwi kuwekeza katika biashara zinazohusiana na pombe, kamari, bidhaa za nguruwe au sekta nyingine zilizokatazwa katika Uislamu.

Kwa mtazamo wa Kiislamu, mali ni amana kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hivyo, kuikuza mali kwa njia halali ni sehemu ya wajibu wa mtu katika kusimamia rasilimali alizopewa.

Aina za uwekezaji halali

Mfumo wa fedha za Kiislamu umeendelea kutoa chaguo mbalimbali za uwekezaji zinazokubalika katika Sharia. Vyombo hivi vinawawezesha watu kukuza mali zao huku wakizingatia maadili ya dini.

Moja ya chaguo hizo ni amana za Kiislamu. Hizi ni bidhaa za benki zinazotumia mfumo wa kugawana faida unaoitwa mudaraba, ambapo mteja huweka fedha na benki huzisimamia katika shughuli halali za biashara. Faida inayopatikana hugawanywa kwa uwiano uliokubaliwa.

Dhahabu pia ni mojawapo ya uwekezaji unaokubalika. Kwa muda mrefu dhahabu imekuwa mali inayotumika kuhifadhi thamani ya fedha. Wawekezaji wengi huitumia kama kinga dhidi ya mfumuko wa bei na misukosuko ya kiuchumi.

Pia kuna hisa za Sharia, ambazo ni hisa za kampuni zinazofanya shughuli halali za biashara. Kampuni hizi huchujwa ili kuhakikisha hazijihusishi na sekta zilizokatazwa kama pombe, kamari au huduma za kifedha zinazotegemea riba.

Sukuk ni chombo kingine muhimu cha uwekezaji wa Kiislamu. Mara nyingi hufananishwa na hati fungani, lakini tofauti yake ni kwamba mapato yake hayatokani na riba bali kutokana na faida ya mali au mradi unaofadhiliwa.

Vilevile kuna mifuko ya uwekezaji ya Kiislamu. Hii ni mifumo ya uwekezaji ya pamoja ambapo fedha za wawekezaji hukusanywa na kusimamiwa na wataalamu wa uwekezaji, huku zikielekezwa katika vyombo vinavyokubalika katika Sharia.

Misingi ya huduma za fedha za Kiislamu

Uwekezaji halali unaongozwa na kanuni kadhaa za msingi katika mfumo wa fedha za Kiislamu. Msingi wa kwanza ni katazo la riba. Katika Uislamu, faida halali inapaswa kutokana na shughuli halisi ya kiuchumi kama biashara au uwekezaji wa mali.

Kanuni nyingine ni kuepuka gharar, ambayo ni mikataba yenye utata au kutokuwa na uhakika. Sharia inasisitiza uwazi katika mikataba ili kuondoa udanganyifu na migogoro.

Pia kuna katazo la maysir, yaani kamari au ubashiri wa kifedha. Shughuli zinazotegemea bahati badala ya shughuli halisi za kiuchumi hazikubaliki katika mfumo wa fedha wa Kiislamu.

Aidha, uwekezaji lazima ufanyike katika sekta halali pekee. Hii inalenga kuhakikisha kuwa fedha hazitumiki katika biashara zinazokiuka maadili ya Kiislamu.

Kwa ujumla, misingi hii inalenga kujenga mfumo wa kifedha unaozingatia haki, uwazi na uwajibikaji katika shughuli za kiuchumi.

Mbinu za uwekezaji halali

Mbinu za uwekezaji halali zinahusisha kanuni kadhaa za vitendo ambazo zinaweza kumsaidia mwekezaji kufanya maamuzi sahihi. Kanuni ya kwanza ni kuhakikisha uwekezaji unaofanywa ni halali na unaendana na mafundisho ya Uislamu.

Nia pia ina nafasi muhimu katika uwekezaji. Mtu anaweza kuwekeza kwa nia ya kulinda familia yake, kusaidia jamii au kujenga ustawi wa muda mrefu.

Ni muhimu pia kuwekeza kwa kiasi kinacholingana na uwezo wako wa kifedha. Kabla ya kuwekeza, ni vyema kuwa na akiba ya dharura ili kukabiliana na changamoto za kifedha zisizotarajiwa.

Wawekezaji wanashauriwa pia kuwa na mtazamo wa muda mrefu. Uwekezaji wa muda mrefu mara nyingi hutoa nafasi kubwa ya ukuaji wa mali kuliko ule unaolenga faida ya haraka.

Kugawanya uwekezaji katika mali mbalimbali ni mbinu nyingine muhimu. Njia hii husaidia kupunguza hatari kwa sababu hasara katika uwekezaji mmoja inaweza kufidiwa na mafanikio katika mwingine.

Mwekezaji pia anapaswa kufanya utafiti wa kutosha kabla ya kuwekeza ili kuepuka udanganyifu au miradi isiyo na msingi.

Katika mtazamo wa Kiislamu, mali pia inapaswa kutakaswa kupitia zaka na sadaka. Hii si tu wajibu wa kidini bali pia njia ya kuhakikisha mali inakuwa na baraka.

Pia ni vyema kumwomba Mwenyezi Mungu mwongozo kupitia dua au swala ya istikhara kabla ya kufanya maamuzi makubwa ya kifedha.

Hatimaye, kuwa na moyo wa shukrani na kutoa katika njia ya Mungu ni sehemu ya falsafa ya uwekezaji wa Kiislamu. Mfumo huu hauishii kuongeza mali pekee, bali unalenga kujenga ustawi wa kifedha unaoendana na maadili ya dini na manufaa ya jamii.